





## TMA yatoa ufafanuzi kuhusu mvua kuchelewa

UKURASA 3



## LAPORTA: HATUWAWEZI HAALAND NA MBAPPE

UKURASA 21


# Nipashe

Jumatano Machi 30, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580900

www.ippmedia.com

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US




Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela (kushoto), akibadilishana mikataba ya makubaliano ya mkopo na dhamana za mikopo ya Sh. bilioni 182 na Mkurugenzi Mkuu wa Proparco Afrika Mashariki, Jean Bendit-Du Chalard, baada ya kutiliana saini, Dar es Salaam jana, kwa ajili ya kuwawezesha wajasiriamali. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Aliyeitaka nafasi ya IGP awekwa kando

• **Jeshi** laanza kumchunguza... *Ukurasa 2*

## YALIYOMO


**UKURASA WA 3**

### UMETIMU WAKATI KUUJUA UHALISIA WA RAIS SAMIA

KAMA siyo leo, basi kesho baadhi ya viongozi wataijua 'rangi halisi' ya Samia Suluhu Hassan, Rais wa Sita wa Tanzania na Rais wa kwanza...

**UKURASA WA 3**

### MWILI WA PROF. NGOWI KUZIKWA KWAO KIBOSHO

MWILI wa aliyekuwa Mkuu wa Chuo Kikuu Mzumbe Kampasi ya Dar es Salaam, Prof. Honest Ngowi unatarajiwa kuzikwa kijijini kwao...

**UKURASA WA 4**

### MAMA AANGUA KILIO HUKUMU DHIDI YAKE

MKAZI wa Kahama, Mary Joseph (51), aMangua kilio katika Mahakama ya Wilaya ya Geita baada ya kuhukumiwa kifungo cha miaka...




Rais Samia Suluhu Hassan akishiriki Mkutano wa 19 wa Wakuu wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), uliofanyika kwa njia ya mtandao, Ikulu Chamwino, jijini Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

## DRC rasmi mwanachama wa saba EAC

UKURASA 2



## Ajali nyingine yaua watu sita, yajeruhi

UKURASA 2

**MICHEZO** **PABLO BADO YUPO SANA SIMBA** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Aliyeitaka nafasi ya IGP awekwa kando

**Na Romana Mallya**

JESHI la Polisi limemhamishia makao makuu aliyekuwa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Kamishna Msaidizi wa Polisi (ACP), Wankyo Nyigesa, huku likitangaza uchunguzi dhidi yake kutokana na maneno anayodaiwa kuyatoa Jumamosi iliyopita mkoani Pwani.

Taarifa ya jeshi hilo iliyotolewa jana na Msemaji wake, David Misime, ilibainisha kuwa Mkuu wa Jeshi la Polisi, IGP Simon Sirro, amefanya uhamisho huo ili kupisha uchunguzi wa maneno (bila kuyataja) yanayodaiwa kutolewa Jumamosi mkoani Pwani na kamanda huyo wakati wa sherehe ya kumuaga.

"Uhamisho huu umefanyika ili kupisha uchunguzi wa tukio la Machi 26, mwaka huu, katika sherehe ya kumuaga aliyekuwa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani ambapo alitoa maneno ambayo yanaonyesha kuwapo na ukiukwaji wa nidhamu kulingana na miongozo ya Jeshi la Polisi.

"Suala hili limeanza kufanyiwa kazi na matokeo ya uchunguzi huo yatafikishwa katika mamlaka za kinidhamu kwa hatua zaidi," Misime alisema katika taarifa yake hiyo.

Wiki iliyopita, Jeshi la Polisi lilifanya mabadiliko madogo ya makamanda na miongoni mwa walioguswa alikuwa ni Kamanda Nyigesa ambaye alitolewa Pwani kwenda kuwa Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Kagera.

Ikiwa ni siku tatu tangu Kamanda Nyigesa kuagwa Mkoa wa Pwani ili kwenda kutumikia Mkoa wa Kagera, jana IGP Sirro, alitangaza mabadiliko mengine na kumgusa Kamanda Nyigesa ambaye amehamishia Makao Makuu ya Polisi Dodoma.

Katika uhamisho na mabadiliko yaliyofanywa na IGP Sirro, pia yamemgusa aliyekuwa Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Rukwa (Kamishna Msaidizi wa Polisi (ACP), William Mwampagale, ambaye amechukua nafasi iliyoachwa wazi na Kamanda Nyigesa mkoani Kagera.

"Aliyekuwa Ofisa Mnadhimu wa Mkoa wa Rukwa, Kamishna Msaidizi wa Polisi (ACP) Theopista Mallya anakuwa Kamanda wa Polisi wa mkoa huo, kuchukua nafasi ya Kamishna Msaidizi wa Polisi Mwampagale ambaye amehamishiwa kwenda kuwa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kagera," ilibainisha zaidi taarifa hiyo.

Vilevile, aliyekuwa Mkuu wa Operesheni Mkoa wa Rukwa, Kamishna Msaidizi wa Polisi (ACP) Mashenene Mayila, anakuwa ofisa mnadhimu wa mkoa wa huo.

Ingawa taarifa ya jana ya Jeshi la Polisi haikutaja maneno halisi aliyoyatamka katika siku tajwa, juzi kulisambazwa video ikiwa na sauti na sura inayodhaniwa ya ACP Wankyo akitamka:

"Mi naomba nifanye miaka mitatu tu halafu baadaye nimwambie mama 'mimi nakukabidhi naondoka, unaonaje hapo?'" Alisema Nyigesa huku watu waliohudhuria hafla hiyo wakiangua vicheko.

Alisisitiza kwamba IGP aliyepo madarakani, Simon Sirro hajafanya makosa, anafanya mambo mazuri lakini yeye atafanya mazuri zaidi.

"Unajua binadamu lazima 'utarget' ya mbele, kuwa na ndoto kubwa, sasa huwezi kuwa na ndoto kwamba nitaendelea kuwa kamanda, mimi nataka kuwa nafasi hizo, kamishna, IGP ili baadaye nifanye makubwa ambayo nimeyafanya."



Vijana wakipaa samaki wa wateja wao, ili kujipatia ujira wa siku katika soko la Feri, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA.**

# DRC rasmi mwanachama wa 7 EAC

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WAKUU wa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), katika kikao chao cha 19 wameipitisha rasmi nchi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) kuwa mwanachama wa jumuiya hiyo.

Kikao hicho kilichofanyika kwa njia ya mtandao chini ya Mwenyekiti wake Rais wa Kenya, Uhuru Kenyatta, kwa kauli moja wameipitisha rasmi Congo kuwa mwanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na umoja huo kufikisha nchi wanachama saba zinazounda umoja huo.

Wakuu wengine ni pamoja na Rais Samia Suluhu wa Tanzania, Rais Yoweri Museven wa Uganda, Rais Paul Kagame wa Rwanda, Prosper Bazombanza Makamu wa Rais Burundi na Sudan ya Kusini iliwakilishwa na Dk. Barnaba Marial Benjamin, waziri anayeshughulikia masuala ya Rais Sudani Kusini.

Kwa upande wake Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Dk. Peter Mathuki, akizungumza na waandishi wa habari alisema tukio hilo ni kubwa na heshima kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki kuialika rasmi Congo kuwa mwanachama mpya wa jumuiya hiyo.

"Siku ya leo kwetu ni kubwa ya heshima wakuu wa nchi za EAC wameitikia rasmi Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo kuwa mwanachama wa Jumuiya hiyo," alisema.

Alisema ni furaha yao na wananchi kupitia kujiunga kwa Congo kutaongeza fursa za kiuchumi na kibiashara katika kusafirisha bidhaa kuanzia Bahari ya Hindi hadi Bahari ya Atlantiki.

Alisema nchi hizo zikikubaliana kuondoa vikwazo mipakani katika biashara zitaongeza nafasi kwa wananchi wa Jumuiya hiyo.

Kwa sasa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki zinakadiriwa kuwa na raia wapatao milioni 193 na kujiunga kwa Congo kutaongeza idadi hiyo na kufikia watu milioni 280 na kufanya mwingiliano wa kibiashara kuwa mkubwa zaidi.

Akizungumzia masuala ya kiusalama katika nchi hiyo alisema nchi hizo zitafanya jitihada za pamoja kuunganisha nguvu kuhakikisha wanadumisha usalama na amani katika nchi hiyo.

"Sisi kwa pamoja tutajitahidi kuwasaidia kuona Jamhuri ya Congo inaondokana na changamoto za kiusalama zilizopo katika nchi hiyo kwa umoja wetu kama nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki," alisema.

# Ajali nyingine yaua watu sita, yajeruhi

**Na Hamida Kamchalla,** LUSHOTO

WATU sita wamefariki dunia na wengine kujeruhiwa baada ya gari walilokuwa wakisafiria kuacha njia na kutumbukia korongoni jana asubuhi.

Kamanda wa Polisi mkoani Tanga, Safia Jongo, alisema jana kuwa tukio hilo lilitokea majira ya asubuhi kwenye eneo la Nyasa (Soni) - Mombo wilayani Lushoto, likihusisha gari aina ya Fuso lenye namba za usajili T 239 AFB lililokuwa limebeba bidhaa za sokoni kutokea Lushoto kwenda wilayani Handeni.

Kamanda Jongo alibainisha kwamba kwa taarifa za awali, watu wanne walifariki papo hapo na baadaye waliongezeka wawili kutoka miongoni mwa majeruhi wa ajali hiyo.

"Waliotutoka mwanzoni walikuwa wanne, lakini baadaye waliongezeka majeruhi wawili na jumla kufikia watu sita ambapo kati ya hao wanaume ni wanne na wanawake ni wawili," alifafanua.

Kamanda Jongo aliwataja waliofariki dunia kuwa ni: Juma Mohamedi na Mwajuma Hatibu, wote wakazi wa Handeni; Jumanne Adam, mkazi wa Soni; Mohamedi Makakala, mkazi wa mjini Handeni; Zaina Ramadhani, mkazi wa Kwamkono Handeni na maiti ya mtu mmoja ilikuwa haijatambuliwa.

Pia aliwataja majeruhi kuwa ni pamoja na Rasuli Makalala, mkazi wa Kijiji cha Komwale wilayani Handeni; Mussa Kajia, mkazi wa Lukozi mjini wilayani Lushoto; Rumisha Msagati, mkazi wa Wena Bumbuli; Amina Mhina, mkazi wa Handeni; Mwajabu Mpulizi, mkazi wa Chogo, Handeni; na Mama Latifa, mkazi wa Handeni.

"Watumiaji wa vyombo vya moto mkoani hapa, kuweni makini pindi mnapokuwa barabarani, endeleeni kufuata sheria, kanuni na taratibu za usalama barabarani," alisema Kamanda Jongo.

HABARI KITAIFA

# Mwili wa Prof. Ngowi kuzikwa kwao Kibosho

**Na Mwandishi Wetu**

MWILI wa aliyekuwa Mkuu wa Chuo Kikuu Mzumbe Kampasi ya Dar es Salaam, Prof. Honest Ngowi, unatarajiwa kuzikwa kijijini kwao Singa, Kata ya Kibosho mkoani Kilimanjaro.

Prof. Ngowi alifariki dunia juzi asubuhi katika ajali iliyohusisha magari matatu eneo la Miwaleni Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha mkoani Pwani.

Kwa mujibu wa baba mdogo wa marehemu, Thomas Ngawaiya, kikao kilichotarajiwa kufanyika jana jioni nyumbani kwa Prof. Ngowi Mbezi Makabe mkoani Dar es Salaam ndicho kilitarajiwa kutoka na ratiba kamili ya lini mwili huo bingwa wa uchumi utazikwa.

Ngawaiya alibainisha kuwa mwili wa mwanawe ulikuwa umetolewa Hospitali ya Mkoa wa Pwani (Tumbi) Kibaha na kupelekwa Hospitali ya Jeshi ya Lugalo mkoani Dar es Salaam.

Juzi, Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Pwani, Pius Lutumo, alisema ajali hiyo ilihusisha gari lenye namba za usajili T 608 AGV likiwa na tela lenye namba T 317 AQM aina ya Scania ambalo lilihama upande wake wa barabara na kugonga gari T 256 CMF aina ya Noah lililokuwa likitoka Dar es Salaam kwenda Morogoro.

Alisema baada ya Scania hilo lililokuwa ikitoka Congo kwenda Dar es Salaam kugonga Noah, lilisababisha kontena kuchomoka na kuliangulia gari lenye usajili SU 38223 aina ya Toyota Land Cruiser, lililokuwa likitoka Dar es Salaam kwenda Morogoro na kusababisha kifo cha Prof. Ngowi na dereva wake, Innocent Gerson.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akizungumza kwenye mkutano wa wadau wa zao la kahawa, Kayanga, Karagwe mkoani Kagera jana. Wapili kushoto ni Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe na watatu kushoto ni Katibu Tawala wa Mkoa wa Kagera, Prof. Faustin Kamuzora. **PICHA: OWM**

# Umetimu wakati kuujua uhalisia wa Rais Samia

**Na Sanula Athanas**

KAMA siyo leo, basi kesho baadhi ya viongozi wataijua 'rangi halisi' ya Samia Suluhu Hassan, Rais wa Sita wa Tanzania na Rais wa kwanza mwanamke Afrika Mashariki.

Kwa nini? Iko hivi: Jijini Dodoma Oktoba 10, mwaka jana, Rais Samia alizindua mpango wa maendeleo kwa ustawi wa taifa na mapambano dhidi ya ugonjwa wa UVIKO-19.

Siku hiyo, Rais Samia aliwaonya watakaodokoa fedha za mkopo wa kukabiliana na athari za UVIKO-19 (Sh. trilioni 1.3) kuwa waitajua rangi yake halisi na hatakuwa na huruma na mtu.

Katika kutilia mkazo angalizo lake hilo, Rais Samia akamwagiza Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kufuatilia kwa karibu matumizi ya fedha hizo ili zitumike kwa malengo yaliyokusudiwa na thamani halisi.

"Hili niliseme tu kwa wale watakaotaka kujua rangi zangu halisi, mkinitizama hivi mnasema Mheshimiwa Rais ni mweupe lakini nina rangi halisi. "Kwa hiyo, kwa wanaotoka kuzijua rangi zangu, wajaribu kudokoa fedha hizi au wabadilishe matumizi bila maelewano.

"Sitakuwa na huruma na mtu atayechezea fedha hii kuanzia mawaziri wangu, chini kwa wakurugenzi na wanaowafuata. Niwaombe mkasimamie vyema miradi hii," alionya.

Siku hiyo, Rais Samia pia aliagiza kufanyike ukaguzi wa fedha zote zilizotumika kwenye miradi yote mikubwa, akisisitiza kuwa miradi ya kimkakati ni urithi ulioachwa na Hayati Dk. John Magufuli.

Katika kutekeleza maagizo ya Rais, Machi 3, mwaka huu, CAG, Charles Kichere, aliweka wazi kwamba ofisi yake imefanya ukaguzi maalumu wa matumizi ya fedha za UVIKO-19 zilizopelekwa kwenye halmashauri nchini.

"Tunampongeza Mheshimiwa Rais Samia kwa namna anavyokabiliana na janga la Uviko-19, ninampongeza Rais kwa namna alivyotoa maelekezo ya matumizi ya fedha za kukabiliana na Uviko-19, hususan afya, elimu, maji na hatua anazochukua za kudhibiti matumizi ya fedha hizo," alisema.

CAG Kichere alibainisha kuwa katika kuunga mkono jitihada hizo, ofisi yake imetekeleza jukumu lake la kikatiba kwa kufanya ukaguzi kwenye halmashauri zilizopata fedha hizo.

"Tukaguzi wa fedha hizo zote za UVIKO-19 zilizoletwa na Mheshimiwa Rais na kila senti ya fedha hizo itakaguliwa na taarifa itatolewa, ili kuhakikisha fedha hizo zimetumika kulingana na maelekezo, taratibu, sheria na miongozo ya matumizi ya fedha za umma," alisema.

**MUDA UMETIMIA**

Ibara ya 143(4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inamtaka CAG kuwasilisha kwa Rais taarifa juu ya ukaguzi wa hesabu za Serikali ya Jamhuri ya Muungano, hesabu zinazosimamiwa na watumishi wote wa serikali, hesabu za mahakama na hesabu zinazosimamiwa na Katibu wa Bunge.

Baada ya kupokea taarifa hiyo, imeelekezwa na katiba hiyo kwamba Rais atawaagiza watu wanaohusika wawasilishe taarifa hiyo kwenye kikao cha kwanza cha Bunge kitakachofanyika baada ya Rais kupokea taarifa hiyo na itabidi iwasilishwe katika kikao hicho kabla ya kupita siku saba tangu siku ile kilipoanza kikao hicho.

Mkutano unaofuata wa Bunge ni mahusus kwa ajili ya bajeti ya serikali kwa mwaka ujao wa fedha uliopangwa kuanza Aprili 5, mwaka huu jijini Dodoma.

Ni katika mkutano huo wa Bunge ripoti ya ukaguzi wa CAG kwa mwaka wa fedha 2020/21 itawasilishwa, hivyo ni wazi kwamba kati ya leo na kesho, Rais atapokea ripoti hiyo ya ukaguzi kutoka kwa mdhibiti huyo.

# TMA yafafanua mvua kuchelewa

**Na Faustine Feliciane**

MAMLAKA ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) imetoa ufafanuzi kuhusu kuchelewa kunyesha kwa mvua kwenye baadhi ya maeneo licha ya utabiri wake wa awali kutahadharisha kuwa ingenyesha mvua kubwa wiki ya tatu na ya nne ya mwezi Februari mwaka huu.

TMA imesema licha ya mvua kuanza kunyesha kama ilivyotarajiwa mwezi Februari, kumetokea vipindi virefu vya ukavu kuanzia wiki ya kwanza ya mwezi Machi hususani kwa baadhi ya maeneo ya nyanda za juu Kaskazini Mashariki na Ukanda wa Pwani ya Kaskazini Mashariki.

Imesema hali hiyo imesababishwa na uwapo wa vimbunga hususani Kimbunga Gombe kilichodumu kwa muda mrefu katika Bahari ya Hindi eneo la rasi ya Msumbiji.

Taarifa ya mamlaka hiyo kwa vyombo vya habari jana, ilibainisha kuwa mbali na kimbunga hicho, pia kujitokeza kwa joto la bahari la chini ya wastani katika eneo la Pwani ya Afrika Mashariki kumechangia kuchelewesha mvua.

"Hali hii pia imechangia ukanda mvua (ITCZ) kuendelea kusalia maeneo ya kusini mwa nchi yetu ambapo kwa kawaida mwanzoni mwa mwezi Machi huanza kuelekea maeneo ya kaskazini mwa nchi yetu. Hizi zote ni sababu za mvua kuchelewa ," TMA ilifafanua zaidi katika taarifa yake hiyo.

Hata hivyo, mamlaka hiyo ilibainisha kuwa unyeshaji wa mvua unatarajiwa kuimarika katika baadhi ya maeneo mwishoni mwa mwezi Machi na mwanzoni mwa mwezi ujao na kufuatiwa na upungufu wiki ya pili ya mwezi Aprili.

"Lakini kutokana na ukanda wa mvua kuendelea kusalia kusini mwa nchi yetu, kumesababsha mvua za msimu kuendelea kunyesha kwa kiwango cha kuridhisha kwa maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka (Kigoma, Dodoma, Singida, Tabora, Ruvuma, baadhi ya maeneo ya Mkoa wa Morogoro pamoja na nyanda za juu Kusini Magharibi).

TMA imewataka wananchi kuendelea kufuatilia taarifa za hali ya hewa inazozitoa kila wakati ili kufahamu mwenendo wa mvua na hali ya hewa kwa ujumla.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe:@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470 DODOMA,

**TANGAZO**

1. Ndugu Wananchi mnatangaziwa kua siku ya tarehe **24.03.2022** mnatangaziwa hadi **05.04.2022** kampuni ya **Spedag Interfreight** itasafirisha mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **Holili** kuelekea **Moshi**, gari hilo lenye namba za usajili: **KDB189J / ZG5310 KCW051Z / ZG2320 KCW052Z / ZG3212 KBQ 628Z / ZE 0941**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| **Urefu** | - | **Mita 28.4** |
| **Upana** | - | **Mita 5.0** |
| **Kimo** | - | **Mita 5.6** |

3. Njia itakayotumika: **Holili hadi Moshi kupitia Soweto,** gari litasafiri muda wa mchana tu ( **Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 jioni)**

*Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.*

216769502

# Wakulima kahawa Kagera wapunguziwa kero ya tozo

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ametangaza uamuzi wa serikali wa kuondoa tozo 42 kati ya 47 ambazo wakulima wanatozwa wakulima wa kahawa wa Mkoa wa Kagera, hivyo kubakia tozo 5 tu.

Sasa tozo itakuwa ni jumla ya Sh. 267 kwa kila kilo ya kahawa, kutoka Sh. 830 za awali.

Waziri Mkuu ametoa maamuzi hayo kufuatia tume maalum aliyoiunda ili kupitia utaratibu na mfumo wa uendeshaji wa vyama vya ushirika wa zao la kahawa mkoani Kagera.

Majaliwa amewaagiza viongozi wa vyama vya ushirika, wasimamie vyama vyao kwa uaminifu na weledi ili vilete tija kwa wakulima.

Pia amewataka viongozi wa vyama vikuu vya ushirika kuacha tabia ya kukopa pesa benki kwa ajili ya kununua kahawa kwa wakulima.

Waziri Mkuu alitoa maagizo hayo jana alipoendesha mkutano maalum wa wadau wa zao la kahawa mkoani Kagera uliofanyika wilayani Karagwe.

Alisema kuanzia sasa mauzo ya kahawa katika Mkoa wa Kagera yatafanyika kwa njia ya mnada. "Mnada huo utafanyika kwenye ngazi ya vyama vya msingi."

Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, alisema baadhi ya vyama vya ushirika vimekuwa vikiwaumiza wakulima wa kahawa kwa kuwaongezea tozo zisizokuwa na tija.

Amesema jambo hilo linafanyiwa kazi kwani wakulima wa kahawa mkoani Kagera wamekuwa wakilia na tozo kubwa zaidi ya 47 na bado wamekuwa wakicheleweshewa malipo.

Waziri huyo amemwagiza Mkurugenzi wa Bodi ya Kahawa kugawa miche ya kutosha ya kahawa kwa wakulima ili ilete tija na kuwaongezea kipato.

Alisema ili kuhakikisha maofisa ugani wanatekeleza majukumu yao ipasavyo wizara imeandaa utaratibu wa kutoa usafiri pamoja na vifaa vya kupimia udongo.

Awali, Katibu Tawala wa Mkoa wa Kagera, Prof. Faustin Kamuzora, alisema katika msimu wa kilimo wa mwaka 2021/2022 mkoa ulizalisha jumla ya tani 52,000 za kahawa ya maganda iliyokuwa na thamani ya Sh. bilioni 69.

"Bei ya kahawa imeendelea kuimarika kwani katika msimu huu wakulima walilipwa shilingi 1,300 kwa kilo moja ya kahawa ya maganda na Sh. 3,300 kwa kilo moja ya kahawa hai (Organic cofee)."

Naye Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais-TAMISEMI, Innocent Bashungwa, alisema kutokana na usimamizi mzuri wa serikali katika zao la kahawa, tayari wakulima wemeanza kuona manufaa kwani bei ya zao hilo imepanda.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Tume Maalumu ya kuchunguza mwenendo wa zao hilo, Dk. Fabian Magawa Madele, alisema katika uchunguzi waligundua ubadhirifu wa zaidi ya shilingi bilioni saba ambazo zilitumika nje ya utaratibu wa vyama vya ushirika.



Ofisa miliki wa Wakala wa Majengo Tanzania (TBA), Emmanuel Pesambili, akifungua moja ya vyumba vya majengo ya Magomeni Kota na kumkabidhi mmiliki wa chumba hicho, John Mussa (kushoto), wakati wa ugawaji wa nyumba kwa wakazi husika, mkoani Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## RUSHWA MGODINI

# Mama aangua kilio hukumu dhidi yake

**Na Joctan Ngelly, GEITA**

MKAZI wa Kahama, Mary Joseph (51), ameangua kilio katika Mahakama ya Wilaya ya Geita baada ya kuhukumiwa kifungo cha miaka mitatu jela au kulipa faini ya Sh. milioni moja kwa kosa la kumhonga Ofisa Rasilimali Watu wa Geita Gold Mining Limited (GGML), Dominick Marando, Sh. 520,000 ili mwanawe, Elizabeth Rugendo, apate kazi ya ulinzi katika mgodi huo.

Hukumu hiyo ilitolewa jana na Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Samweli Maweda, baada ya mshtakiwa huyo kukiri kutenda kosa hilo.

Hakimu Maweda baada ya mshtakiwa huyo kukiri kosa lake hilo, alimwambia Wakili Mwandamizi wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Geita, Antidius Rwakatale, amsomee mshtakiwa huyo maelezo ya awali.

Akisoma maelezo ya awali, wakili huyo alidai kuwa Febuari 21, mwaka huu, GGML walikuwa wametangaza nafasi ya kazi ya ulinzi na Elizabeth Rugendo alikuwa ameomba nafasi hiyo ya ulinzi.

Alidai kuwa baada ya mtoto wa mshtakiwa kuomba kazi ya ulinzi GGML, mshtakiwa alimtumia fedha Sh. 520,000 kwenye simu ya Ofisa Rasilimali Watu wa GGML, Dominick Marando kwa njia ya M-Pesa ili mtoto wake huyo apate kazi ya ulinzi kwenye mgodi huo.

Alidai kuwa baada ya fedha hizo kuingia kwenye akaunti ya M-Pesa ya Ofisa Rasilimali Watu wa GGML, Febuari 21 mwaka huu, ofisa huyo alikwenda moja kwa moja kutoa taarifa ofisi ya TAKUKURU Mkoa wa Geita.

Wakili huyo aliendelea kudai kuwa baada ya taarifa hizo kuwasilishwa, Machi Mosi, mwaka huu, mshtakiwa huyo alikamatwa na alipohojiwa, alikiri kutuma fedha hizo kwa ofisa huyo wa GGML ili kushawishi mtoto wake apatiwe kazi ya ulinzi kwenye mgodi huo.

Hakimu Maweda alisema kwa kuwa mshtakiwa amekiri kosa mwenyewe bila kulazimishwa na mtu yeyote, hivyo mahakama hii inamtia hatiani kwa kosa hilo na kumtaka ajitetee ili kumpunguzia adhabu.

Mshtakiwa huyo aliangua kilio mahakamani na kudai kuwa yeye ana watoto watatu wanaomtegemea kwa sababu mume wake amemtelekeza na kumwacha anahangaika na watoto, pia anafanya ujasiriamali, hivyo anaomba mahakama hiyo impunguzie adhabu.

Upande wa Jamhuri ukiongozwa na Wakili Mwandamizi wa TAKUKURU, Rwakatale, uliiomba mahakama hiyo itoe adhabu kali kwa mshtakiwa huyo ili iwe fundisho na kupunguza wimbi la rushwa kwenye ajira za taasisi za serikali na kampuni za watu binafsi.

"Pia tunaomba fedha hizo Sh. 520,000 zitaifishwe ili zirudi serikalini," wakili huyo alidai.

Akisoma hukumu, hakimu huyo alisema ajira za kununua zimekuwa nyingi mkoani Geita na kufanya watu wenye elimu kukosa kazi kwa kuwa hawana fedha.

Alisema suala la kutelekezwa na mume halihalalishi kununua ajira GGML kwa kuwa ajira za kununua zinasababisha mtoto wa maskini kukosa kazi kutokana na kutokuwa na fedha, hivyo wenye fedha ndiyo wanaopata kazi.

Hakimu Mawenda alitupilia mbali utetezi huo wa mshtakiwa na kusema kitendo ulichokifanya siyo kizuri, hivyo mahakama inamuhukumu miaka mitatu jela au kulipa faini ya Sh. milioni moja.

Hakimu huyo pia alisema Sh. 520,000 alizokuwa umemtumia Ofisa Rasilimali Watu wa GGML zitaifishwe na zipelekwe serikalini na kama kuna upande ambao haujaridhika na hukumu, rufani iko wazi.

Baada ya Hakimu huyo kumaliza kusoma hukumu hiyo, mshtakiwa aliangua kilio, akiomba apunguziwe faini, akitamka: "Mimi milioni moja sina, nina laki tano tu".

Hata hivyo, Hakimu Maweda aliamru mshtakiwa huyo atolewe ndani ya chumba cha mahakama na baadaye mshtakiwa huyo alifanikiwa kulipa faini hiyo ya Sh. milioni moja na kuachiwa huru.

## 100 Magomeni Kota wakabidhiwa nyumba

**Na Christina Mwakangale**

WAKAZI wa Magomeni Kota 100 kati ya 644, wamekabidhiwa funguo, huku wazee wakipewa kipaumbele, ikiwa ni awamu ya kwanza ya makabidhiano hayo ambayo yatachukua siku 10 kabla ya kuanza kuingia rasmi kwenye nyumba zao.

Idd Kibwana (82), mmoja wa wakazi hao akizungumza na waandishi wa habari, jana mkoani Dar es Salaam, baada ya kukabidhiwa funguo, alisema alisubiri hatua hiyo kwa takribani miaka 11, tangu wakazi hao walipoondolewa kwenye makazi ya zamani.

"Mimi kwangu hii ni hatua kubwa kwa sababu mwenzangu (mkewe) niliyeanza naye harakati hizi ameshaondoka, ninashukuru.

Kibwana ambaye ameishi kwenye makazi ya Magomeni ya zamani tangu Machi, mwaka 1960 akipanga eneo hilo akiwa bado kijana hadi alipooa hapo baadaye.

"Mimi nilikuwa dereva wa makampuni mbalimbali zamani, Tanesco, Airport, hadi nikastaafu 2015, nilipopata ajali ya gari. Binti yangu wa kwanza amezaliwa kwenye kota za zamani, hadi sasa nina wajukuu wengi," alisema Kibwana.

Mwajuma Mtambo (65), alisema amefurahi kukabidhiwa funguo na kuwa mkazi wa makazi hayo mapya, akisema akiwa na mama yake waliishi kwenye kota za zamani tangu mwaka 1972 na baada ya kufariki mzazi wake, akarithi.

"Mama yangu alipofariki nikarithi katika kuwa mmiliki halali nikakabidhiwa na serikali. Nashukuru nimepata vyumba viwili, sebule, choo, bafu, jiko, nitafurahi na wajukuu zangu," alisema Mwajuma.

Mwenyekiti wa Wakazi Magomeni Kota, George Abel, alisema kukabidhiwa funguo itakuwa ni kwa awamu ili kuondoa msongamano na kwamba, makabidhiano ya funguo yanaenda sambamba na kujaza fomu na kwamba utapangwa utaratibu wa kuanza kuhamia.

"Gari la tani tatu kuleta mizigo hapa ndio linaloruhusiwa, zaidi ya hapo hairuhusiwi, utasababisha kuharibu mazingira. Wakazi wote wamepewa ofa kukopeshwa mitungi ya gesi ya Taifa Gas kwa kulipia ndani ya mwezi mmoja, maana sio mtu akaanza kupikia kuni hapa, haya ni makazi ya kisasa.

"Usafi pia tunajipanga baada ya ofa ya serikali kwa miezi mitatu kuisha, katika kutufanyia usafi, tunatafuta mkandarasi ambaye atachukua tenda ya kufanya usafi na si wakazi wafanye usafi wenyewe," alisema Abel.

Ofisa Miliki kutoka Wakala wa Majengo Tanzania (TBA), Emmanuel Pesambili, alisema, kila mkazi ambaye anatambulika kuwa ni mpangaji mnunuzi, atahitajika kuwa na kitambulisho kinachoonyesha jina lake linalooendana na lililopo kwenye orodha ya wakazi walio tambuliwa.

"Tumekabidhi funguo kwa wakazi kwa kuanza na watu 100, tunawapangia katika 'block one', wazee tumewapa kipaumbele, ila kuna fomu ambayo itajazwa baada ya kufanyika ukaguzi wa kila kilichomo ndani na kinafanya kazi na itajazwa na wahusika wote. Ili kuthibitisha kama kweli anastahili kukaa katika nyumba hiyo, waje na kitambulisho cha NIDA, cha kupigia kura au leseni ya gari," alisema Pesambili.

Wiki iliyopita, Rais Samia Suluhu Hassan aliuzindua makazi hayo yaliyojengwa na TBA kwa Sh. bilioni 52, na kuwaahidi kukaa bure kwa miaka mitano, na kuruhusiwa kulipa gharama za ujenzi wa nyumba pekee bila ya gharama za ardhi na miundombinu baada ya muda huo.

# Mbarawa atoa miezi 3 ukarabati wa MV. Kazi

**Na Jenifer Gilla**

WAZIRI wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, amemtaka mkandarasi Songoro Marine anayefanya ukarabati katika Kivuko cha MV. Kazi kuhakikisha kivuko hicho kinakamilika ndani ya miezi mitatu.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam, wakati akikagua kivuko hicho Prof. Mbarawa alisema serikali imeshapata fedha kwa ajili ya ukarabati huo, hivyo ni wajibu wa Wakala wa Ufundi na Umeme nchini (TEMESA) na Mkandarasi Songoro Marine kuhakikisha taratibu za manunuzi na mikataba ya kazi hiyo inakamilika kwa haraka.

"Hakikisheni ifikapo Ijumaa ya Aprili Mosi, utaratibu wa mikataba uwe umekamilika na kasi ya ujenzi na uagizaji vifaa nje ya nchi kwa ajili ya kazi hiyo iongezeke ili kufikia lengo," amesisitiza Prof. Mbarawa.

Prof. Mbarawa amesema idadi ya wakazi wa Kigamboni wanaohitaji huduma ya kivuko imekuwa ikiongezeka siku hadi siku hivyo kuwataka TEMESA kutengeneza ratiba maalum ya ukarabati wa vivuko vyake ili kuondoa usumbufu vinapofanyiwa matengenezo.

"Serikali imetenga fedha katika bajeti ijayo ya ujenzi wa kivuko kipya kikubwa kitakachokuwa na uwezo wa kubeba abiria elfu tatu kwa wakati mmoja hivyo TEMESA jipangeni kuendana na kasi ya Serikali," amesisitiza Prof. Mbarawa.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni, Bi. Fatma Almas Nyangasa, amemshukuru Prof. Mbarawa kwa mikakati inayofanywa na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kuboresha huduma za usafiri kwa wakazi wa Kigamboni, na kumuomba aangalie upya viwango vya gharama zinazotozwa kwa mabasi ya abiria yanayotumia Daraja la Nyerere.

"Kupungua kwa gharama za mabasi ya abiria katika Daraja la Nyerere kutapunguza msongamano wa magari katika kivuko cha Magogoni na hivyo kupunguza msongamano kwa kuwa magari mengi yatapita darajani," amesema Bi. Nyangasa.

Naye Meneja wa Ujenzi wa Vivuko TEMESA, Mhandisi Lukombe Kingo'mbe, alimhakikishia Prof. Mbarawa kuwa TEMESA imejipanga kusimamia vizuri ukarabati wa Kivuko cha MV. Kazi na kivuko kipya kitakachoanza kujengwa baadaye mwaka huu.

Zaidi ya abiria 100,000 wanakadiriwa kutumia huduma za vivuko kati ya Kigamboni na Feri kwa siku jijini Dar es Salaam.

# Mfumo kufuatilia mashirika, viwanda vilivyobinafsishwa

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina imekamilisha mfumo rahisi wa kupokea na kutunza kumbukumbu za mashirika ya umma na viwanda vilivyobinafsishwa.

Mfumo huo unaoitwa Ubinafsishaji Information System lengo lake ni_ kufuatilia mafanikio na changamoto za mashirika na viwanda hivyo.

Msajili wa Hazina, Mgonya Benedicto, alibainisha kuhusu mfumo huo wakati wa kikao kazi kati yake na wamiliki na wakurugenzi wa mashirika ya umma yaliyobinafsishwa kilichofanyika jijini Dar es Salaam jana, ikiwa ni mwendelezo wa kikao kingine cha aina hiyo kilichofanyika wiki iliyopita jijini Dodoma.

Alifafanua kuwa, mashirika hayo ya umma yalibinafsishwa ili kuipunguzia serikali mzigo wa kuyaendesha ikiamini kwa kufanya hivyo yangeongeza tija na ufanisi ikiwamo uingizaji wa teknolojia mpya, lakini kubwa zaidi, serikali ililenga kuishirikisha sekta binafsi katika kukuza uchumi wa nchi.

Mgonya alisema mfumo huo upo katika hatua mbalimbali za ukamilishwaji, na kwamba utakapoanza kutumika wawekezaji watateua maofisa wao watakaokuwa na jukumu la kutoa taarifa husika na kusaidia kupunguza safari za maofisa wa serikali kutembelea waliouziwa mashirika hayo. Mashirika takribani 200 kati ya yaliyobinafsishwa, yalifuatiliwa na kufanyiwa tathmini katika mwaka 2021.

Kwa mujibu wa Msajili wa Hazina, kati ya hayo yaliyofuatiliwa imebainika ni mashirika 76 tu yanayofanyakazi vizuri, 41 yanasuasua na 83 hayafanyi kazi na yamefungwa. Aidha kati ya mashirika hayo, viwanda vilikuwa 108, mashamba 54, hoteli 19 na kampuni 19.

Alisema hatua mbalimbali zimechukuliwa ikiwamo kufanya mazungumzo na wawekezaji kuboresha utendaji wa mashirika hayo.

Ikiwa ni mara ya kwanza kwa Msajili wa Hazina kukutana na wawekezaji wa mashirika yaliyobinafishwa ili kubadilishana mawazo katika usimamizi na uendelezaji wa taasisi hizo kwa maslahi mapana ya taifa, Mgonya alisema serikali katika kubinafsisha mashirika, viwanda, mashamba na hoteli ilikuwa na lengo la kuongeza uzalishaji, ufanisi na tija.

Aliwatoa shaka wamiliki na wakurugenzi wa mashirika na viwanda hivyo na kusema wanachofanya wao sio kupanga kuwapora viwanda na mashirika yao, bali kuona kwamba makubaliano yanatekelezwa kwani katika ufuatiliaji pia wamebaini kuwapo kwa kasoro mbalimbali ikiwamo wamiliki kukopa fedha kwa shughuli nje ya uendelezaji wa mashirika yenyewe.

Alisema tangu Ofisi ya Msajili wa Hazina iliporithi majukumu ya lililokuwa Shirika Hodhi la Mali za Mashirika ya Umma (CHC) mwaka 2014 wamekuwa wakitakiwa kufuatilia na kufanya tathmini ili kuona maendeleo ya mashirika na kampuni hizo.

Alisema kutokana na mazingira hayo, serikali inapofanya ufuatiliaji na tathmini haina maana ya serikali kutaka kupokonya mali iliyouzwa au kutaka kuifanya kampuni ilipe kodi kubwa kinyume na sheria, kanuni na taratibu za nchi, bali kubaini changamoto na kusaidia njia za kuzikabili.

Aliwataka wawekezaji hao waliouziwa mashirika, mashamba, hoteli na viwanda vilivyokuwa vya serikali watoe ushirikiano kwa Ofisi ya Msajili wa Hazina wakati inapofanya ufuatiliaji na tathmini ili kwa pamoja changamoto zibainike na njia ya kuzikabili kutafutwa kwa pamoja.

Mwaka 1993 serikali ilianzisha PSRC na kuipa jukumu la kushirikiana na sekta binafsi kurekebisha na kufufua mashirika ya umma yaliyokuwa yanaendeshwa kwa hasara.

Hiyo ilitokana na serikali kuanza kutekeleza mpango wa ubinafsishaji na urekebishaji wa mashirika ya umma mwishoni mwa mwaka 1992 baada ya kufanya marekebisho ya Sheria ya Mashirika ya Umma SURA 257, lengo likiwa kuruhusu sekta binafsi na Watanzania wengi waweze kushiriki katika kumiliki na kuendesha mashirika ya umma ambayo kwa wakati huo yalikuwa hayafanyi vizuri.



Wafanyabiashara wa ng'ombe na mbuzi katika mnada wa Pugu, jijini Dar es Salaam, wakiwa katika kikao cha pamoja na Diwani wa Kata ya Pugu Stesheni, Shabani Mussa, kilichojadili changamoto mbalimbali zinazowakabili katika eneo hilo, jana. **PICHA: MAULID MMBAGA**

# Serikali: Tuipe muda katiba ya sasa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

NAIBU Waziri wa Katiba na Sheria, Godfrey Pinda, amesema Watanzania waipe muda Katiba iliyopo ili iangaliwe maeneo yanayokera ili kuimarishwa, kwa sababu haina tatizo lolote isipokuwa wanaoitafsiri hutoa maana tofauti.

Pinda alitoa msimamo huo jana wakati akizindua magari mawili ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, iliyokabidhiwa kwa ajili ya kutekeleza majukumu yao ya kila siku katika maeneo mbalimbali nchini.

Pinda alisema Katiba hii ni kama Biblia au kitabu chochote cha dini, ambapo kila mmoja akisoma huja na tafsiri tofauti, jambo ambalo linaleta mkanganyiko kwa jamii ambayo husikia na kuichambua vipengele vichache bila kuisoma.

Aliziomba taasisi zote zinazopata nafasi ya kuisemea Katiba kuwa zinapaswa kusaidia kutoa elimu kwa wananchi juu ya uwelewa wa Katiba iliyopo kwa sababu ni mwongozo wa masuala mbalimbali katika utendaji haki za binadamu.

"Naziomba taasisi husika zinapopata nafasi zinapaswa kusaidia kutoa elimu kwa jamii juu ya Katiba iliyopo, hiyo itasaidia watu kuelewa suala la Katiba na sio kutembelea na vipengele viwili na kuvitafsiri tofauti," alisema Pinda.

Alisema kama Katiba ingekuwa mbovu basi serikali ingeshindwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo, na kuwa ndio maana imejikita kutoa elimu kwa jamii ili wapate uwelewa kuhusu Katiba iliyopo na mpya ambayoinazungumziwa.

Alisema serikali inatambua umuhimu ndio maana imeamua kukutana na wadau wa vyama vya siasa kujadili nao.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kasi ajali za barabarani inatisha, idhibitiwe sasa

**NI** mwezi wa tatu tangu kuanza kwa mwaka 2022, lakini kwa kipindi hicho kifupi, ajali za barabarani zimetokea na kukatisha uhai wa baadhi ya watu maeneo mbalimbali nchini na kuacha wengine wakiwa na ulemavu wa kudumu.

Katika ajali za mwezi huu, imo iliotokea mkoani Morogoro iliyosababisha vifo vya watu 22 na nyingine ikiwamo iliyokatisha uhai wa aliyekuwa Mkuu wa Chuo cha Mzumbe, kampasi ya Dar es Salaam, Profesa Honest Ngowi.

Jana asubuhi matukio hayo ya kukatisha uhai wa Watanzania wenzetu yaliendelea baada ya watu sita kufa na wengine kujeruhiwa kufuatia gari walilokuwa wakisafiria kuacha njia na kutumbukia korongoni majira ya asubuhi kwenye eneo la Nyasa (Soni) - Mombo wilayani Lushoto, mkoani Tanga likihusisha gari aina ya Fuso lililokuwa limebeba bidhaa za sokoni kutokea Lushoto kwenda wilayani Handeni.

Hakika, matukio ya kasi ya ajali za barabarani yanasikitisha na kuleta simanzi kutokana na kuondoa nguvu kazi ambayo ni tegemeo la nchi yetu katika mandeleo yake licha ya kwamba siku za nyuma zilionekana kupungua kwa kiwango kikubwa.

Kwa kuwa ajali hizo zinaendelea kupoteza maisha ya watu, tunadhani ni vyema sasa zikachukuliwa hatua madhubuti za kuhakikisha viashiria vyote vinavyoweza kusababisha ajali vinadhibitiwa.

Ni kweli kwamba, ajali haina kinga, lakini tunaamini kuwa viashiria vinaweza kudhibitiwa hasa uzembe wa madereva na mwendo usioruhusiwa unaoweza kumfanya dereva ashindwe kumudu gari na kujikuta akisababisha ajali.

Kwa kiasi fulani, ajali za barabarani zilianza kupungua, lakini ghafla tangu kuanza kwa mwaka huu wa 2022, matukio ya ajali hizo yanazidi kuripotiwa kutoka maeneo mbalimbali nchini kila uchao, hivyo kuzua shaka kwamba kuna wenye dhamana wasiotekeleza majukumu yao inavyotakiwa. Ajali hizo zinatusukuma kushauri Jeshi la Polisi hasa Kikosi cha Usalama Barabarani kukaa na kutafakari na kujitathmini ni kwa nini zimeibuka kwa kasi mwaka huu na kisha hatua zichukuliwe haraka ili kuzikomesha au kuzipunguza.

Kwa maana hiyo, tunadhani ni vyema watakafakari, je, zile tochi ambazo zilikuwa zinatumika kuwamulika madereva wasiozingatia sheria za usalama barabarani zinaendelea kufanya kazi au hapana? Kwa nini ajali zimeibuka ghafla na kwa kasi? Haya ni maswali ya msingi kujiuliza kwa lengo la kujua chanzo cha tatizo hili ni nini.

Iwapo wakatafakari na kisha kuchukua hatua, tunaamini wahusika watakuwa makini wawapo barabarani ili kuhakikisha abiria wanasafiri na kufika kule wanakokwenda bila kukatishwa uhai wao njiani na wengine kupata vilema vya milele.

Tunatambua kazi nzuri inayofanywa na askari wa Kikosi cha Usalama Barabarani, ya kukabiliana na madereva wasiozingatia sheria kwa kuwatoza faini ili waogope na kufanya kazi yao kwa umakini.

Hivyo, tunashauri kasi hiyo iendelee, kwani inawezekana ikawa imepungua na kusababisha ajali kujirudia, lakini abiria nao kwa upande wao ni vyema wasiwe wazito kutoa taarifa mapema wanapoona viashiria vya ajali.


Hapa tunaaminisha kuwa, ili kuwa salama safarini, kila upande ufanye sehemu yake. Madereva wazingatie sheria za usalama barabara, lakini abiria nao kwa upande wao wakemee au kutoa taarifa kwa vyombo husika wanapowaona madereva wakikaidi kufuata sheria, kanuni na taratibu za barabarani.

Kama kila upande utatimiza jukumu lake katika kukabiliana na ajali hizo, tunaamini kasi ya ajali inaweza kupungua kuliko kuendelea kujitokeza mfululizo kama ambavyo imetokea tangu kuanza kwa mwaka huu.

Tunalisisitiza hili kwa umuhimu mkubwa, kutokana na ajali kuchangia katika umaskini wa familia na taifa kwa ujumla.

Ajali nyingi huwa zinaelezwa kuwa chanzo chake ni uzembe wa madereva, tunawashauri wafanye kazi kwa mujibu sheria zinazowaongoza, kwani kwa njia hiyo kuna uwezekano wa kuwafikisha salama abiria kokote waendako.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Malori ya makontena yatembee usiku kunusuru ajali zisizoisha

Na Adam Fungamwango

**KWANZA** kabisa nitoe salamu za rambirambi kwa ndugu, jamaa na marafiki wa msomi wa Chuo Kikuu cha Mzumbe na mchambuzi wa makala mbalimbali za uchumi kwenye vyombo vya habari, Profesa Honest Ngowi na dereva wake, waliofariki dunia juzi yeye pamoja katika ajali ya gari lao.

Pia salamu hizi zifike mbali kwenye mikasa yote ya ajali za magari, kuanzia Mikumi Morogoro wastani wa wiki moja sasa, hadi jana jijini Tanga. Idadi kubwa ya vifo wastani 20.

Marehemu Ngowi na dereva wake walifariki maeneo ya Mlandizi juzi asubuhi baada ya kuangukiwa na kontena lililokuwa kwenye lori alipokuwa akienda Morogoro Kampasi Kuu ya Mzumbe kwenye kikao.

Nitoe pia pole serikalini, kwa wachumi na wanahabari kwa ujumla, kwani taifa limepoteza mtu muhimu kama Ngowi. Ni msomi aliyetegemewa na ajali iliyomzuru ni kwa namna inayozuilika.

Hilo limeshatokea, lakini hadi sasa bado malori yanatembea na makontena yakiwa hayajafungwa kitu chochote.

Hiyo si mara ya kwanza kwa ajali za aina hiyo kutokea. Hadi leo inaonekana bado hatua stahiki hazijachukuliwa.

Taifa kwa jumla limeshapoteza watu wengi kwa namna hii, kuangukiwa na makontena yaliyobebwa kwenye malori. Ajali hizo zimeshawahi kutokea sana Dar es Salaam na hata mikoani, hasa kwenye barabara kuu ya Morogoro au kuelekea Tanga, Moshi na Arusha.

Ilifika hatua hata abiria wakiwa ndani ya mabasi, wakiona wanapishana au kulipita lori lililobeba kontena, au kwenda nalo sambamba barabara moja, basi wanahisi wako hatarini kufika ahera.

Wakati mwingine wanafika hatua kumpigia kelele dereva kuliacha lipite, au alipite ili mioyo yao itulie. Ni hali inayotaka kujirudia.

Imekuwa kawaida sasa, kushuhudia makutano na malori yaliyobeba makontena makubwa barabarani, yawe yametoka bandarini au vyovyote vile.

Ni makontena yanayosafirisha mizigo kutoka jijini Dar es Salaam kwenda mikoani, baadhi nchi za nje kwenye, hadi majirani kama Uganda, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), Zambia na Malawi, mahsusi ni nchi zisizo na bahari.

Mizigo mingi hufungwa kwenye makontema hudhibitiwa kwa kufungwa ili yasianguke na kuhatarisha usalama wa watumiaji wengine barabarani.

Wapo wasafirishaji wanaoyafunga katika namna ambayo hayahatarishi maisha ya waendesha magari binafsi, mabasi ya abiria na hata madereva wenyewe wa malori hayo.

Kinachoonekana, baadhi hawayafungi vema kiasi cha kusababisha maisha ya watu wengine kuwa hatarini.

Ni kawaida makontena hayo hutakiwa kufungwa na nati maalum pande zote nne, hasa kwenye kona zake na ikiwezekana kushikizwa na minyororo, kutegemea ukubwa wa mzigo uliopakiwa.

Unaweza kukutana na lori limebeba kontena likiwa limepachikwa tu, bila ya kufungwa nati au mnyororo hali ambayo ni hatari kwa maisha ya watu kutokana na ukweli kinaweza kuanguka wakati wowote na kusababisha maafa.

Wengine hawayafungi kwa madai yanapelekwa eneo la karibu, hivyo wanaona usumbufu kuyafunga na kufungua kwa muda mfupi.

Wanachojali zaidi ni uharaka kuliko athari zinazoweza kutokea, iwapo litateleza na kuanguka. Mara kadhaa zimetokea ajali za makontena kuanguka na kusababisha maafa, hasa sehemu zenye miinuko, milima, mabonde, na kona kali, kwani makontena huteleza na kwa sababu ni mazito, ama anaweza kuanguka yenyewe, au kusababisha hata lori zima kuanguka.

Wakati mwingine, mtikisiko kwa sababu halijafungwa, husababisha lori kuyumba na kumpotezea mwelekeo dereva.

Kwa kufanya hivyo kunasababisha maisha ya watu, ndani ya lori, watumiaji wengine wa barabara na watembeaji kwa miguu maisha yao kuwa hatarini sehemu yoyote inakopita, kwani lolote linaweza kutokea.

Ni muhimu polisi ikalifuatilia hilo kwa umakini na kuwachukulia hatua kali wote wasiofunga makontena kwenye malori yao, ili kuepusha maafa haya tunayoyashuhudia, ilali yanaepukika. Ni uzembe tu unaopoteza maisha ya watu.

Wamiliki na wanaokodisha malori hayo hawana budi kuhakikisha makontena yanafungwa, ili si tu kuepuka ajali, bali nao kuepuka hasara ya malori yao kuharibika na madhila yanayoambatana na ajali.

Wananchi, pia tuna wajibu kuisaidia polisi kwa kutoa taarifa kama wataona hali hiyo, kwani lisipokukuta wewe litamkuta ndugu, jamaa au rafiki yako.

Mamlaka husika za serikali nazo sasa umefika wakati ziangalie muda wa malori ya makontena kutembea. Ifike wakati yaanze kutembea usiku, muda usio na idadi kubwa ya magari na watembea kwa miguu barabarani.

HABARI KITAIFA

# Kesi wafuasi CHADEMA yaahirishwa

**Na Richard Makore,** MWANZA

VIONGOZI na wafuasi wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) waliokamatwa jijini Mwanza mwaka jana kwa tuhuma za kufanya mkusanyiko usiokuwa halali kanisani, wameendelea kusubiri kwa takribani miezi saba sasa kusomewa maelezo ya awali ya kesi inayowakabili.

Kesi hiyo namba 77 ya mwaka 2021 ilifunguliwa Oktoba 19, 2021 kwenye Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Mwanza na tangu wakati huo washtakiwa wote hawajawahi kusomewa maelezo yao ya awali.

Jana wafuasi hao ambao wapo nje kwa dhamana tangu mwaka jana, walifika tena katika mahakama hiyo lakini kesi yao iliahirishwa kwa madai kuwa mmoja wa washtakiwa hakufika mahakamani kutokana na kuumwa na kulazwa hospitalini.

Mwezi Agosti mwaka jana, wafuasi hao 19 wakiwamo viongozi wa mikoa ya Kanda ya Ziwa, walikamatwa wakiwa kanisani walikodaiwa kwenda kufanya misa ya kumwombea Mwenyekiti wa chama hicho, Freeman Mbowe, aliyekuwa gerezani, akikabiliwa na kesi ya ugaidi.

Akizungumza na Nipashe jana katika mahakama hiyo, Wakili wa washtakiwa hao, Eric Muta, alidai wateja wake hawajasomewa maelezo yoyote ya awali.

Alidai washtakiwa hao wanakabiliwa na tuhuma za kukusanyika bila uhalali katika Kanisa Katoliki la Kawekamo, Jimbo Kuu la Mwanza mwaka jana.

Wakili huyo alidai taratibu za mahakama zimekuwa ndefu, hivyo kusababisha wateja wake kushindwa kuanza kusomewa maelezo ya awali.

Kesi hiyo iko mbele ya Hakimu Mkazi wa Mahakama ya Hakimu Mkazi ya Mkoa wa Mwanza, Bonaventure Lema.

Hakimu Lema aliahirisha kesi hiyo kutokana na mmoja wa washtakiwa kudaiwa kuumwa na imepangwa kutajwa Aprili 13, mwaka huu.

Wakati huo huo, viongozi wa chama hicho Kanda ya Serengeti na Victoria wamelalamikia simu zao pamoja na kompyuta kuendelea kushikiliwa na Jeshi la Polisi mkoani Mwanza.

Katibu wa CHADEMA Kanda ya Victoria, Zakaria Obadia, alisema wao walikamatwa Julai mwaka jana pamoja na Mwenyekiti wao, Mbowe kwa tuhuma za kutaka kufanya mkutano wa kudai Katiba Mpya bila kibali.

Alisema tangu wakati huo, simu zao zimeendelea kushikiliwa na Jeshi la Polisi licha ya Ofisi ya Mwendesha Mashtaka (DPP) kufuta kesi ambayo walikamatwa pamoja na Mbowe.

# Mwenge wa Uhuru kuwang'oa vigogo

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MBIO za Mwenge wa Uhuru mwaka huu zinatarajiwa kuzinduliwa Jumamosi ya wiki hii mkoani Njombe, zikilenga kumulika uovu, uzembe na ufisadi kwenye miradi ya maendeleo inayotekelezwa nchini.

Mbio hizo zitazinduliwa na Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, huku tathmini ya hatua zilizochukuliwa wakati wa mbio hizo mwaka 2021 kwa miradi iliyobainika kuwa na dosari na kesi zilizopo mahakamani, zikiwekwa wazi siku hiyo.

Akizungumza jana na waandishi wa habari jijini hapa, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu), Patrobas Katambi, alisema mbio hizo zimekuwa ni jicho la ziada kwa Rais kwa kumsaidia kuangalia vitendo hivyo na kuchukua hatua kwa viongozi wanaobainika miradi yao kuwa na dosari.

"Katika mbio hizi kuna vijana sita ambao huteuliwa kwa kuzingatia utaalamu, hata mwaka jana mbio zile maalumu ambazo zilikimbizwa na wanajeshi, walikuwamo wahandisi na wataalamu wa fedha," alisema.

Katambi pia lisema timu hiyo ya wakimbiza Mwenge wa Uhuru huambatana na wataalamu wengine kutoka mamlaka mbalimbali na kwa mwaka huu inatarajiwa kufika kwenye mikoa 31 na halmashauri 195, zikibeba ujumbe mkuu ambao ni kuhamasisha wananchi kushiriki sensa ya watu na makazi. "Hata kama kwenye Mwenge hatutakuwa na mhasibu, lakini katika ile timu nyingine ya wanaoambatana nao lazima kuwapo na mtaalamu.

"Niwahakikishie kwenye utaalamu kuna weledi mkubwa. Hawa wakimbiza Mwenge hupitia hatua mbalimbali na wanapopitishwa kwa ngazi ya taifa huwekwa kwenye kambi maalumu na inakuwa ya mafunzo, wanafundishwa masuala ya fedha wakaguaje, nyaraka, miradi ya ujenzi, barabara na wakifuzu ndipo wanapata uteuzi wa kukimbiza Mwenge,"alisema.

Alisisitiza miradi itakayozinduliwa izingatie thamani halisi ya fedha kwa kuwa wanaokimbiza Mwenge huo wana utaalamu wa kutosha wa kufanya ukaguzi.

"Mwenge ni jicho la ziada la Mheshimiwa Rais pamoja na kwamba kote ana vyombo na mamlaka. Kwa hiyo, Mwenge ukipita huko kaa mguu sawa. Kuna neno lilikuwa linasemwa 'ameenda na Mwenge'. Hii ni katika kuhakikisha sheria na taratibu za nchi zinazingatiwa na kutekeleza miradi kwa kusudio lililowekwa," alisema.

Katambi alisema kuna miradi inayokidhi vigezo, huzinduliwa na isiyo na vigezo hukataliwa ili uchunguzi zaidi ufanyike na hatua zichukuliwe.

Akizungumzia miradi 49 yenye thamani ya Sh. bilioni 65.3 iliyokataliwa na Kiongozi wa Mbio za Mwenge mwaka jana ambayo Rais Samia Suluhu Hassan aliagiza uchunguzi wa kina ufanyike na hatua stahiki zichukuliwe kwa wahusika, Naibu Waziri Katambi alisema tayari kuna hatua ambazo zimechukuliwa na Rais kwa viongozi ambao miradi ilikuwa na dosari.

"Kuna wakurugenzi walipoteza nafasi zao, kuna watumishi ambao ni wataalamu walipoteza nafasi zao, kuna wengine kesi zao bado zinaendelea, sasa jambo linapokuwa mahakamani haupaswi kulizungumzia kwa kuwa ndicho chombo pekee cha uamuzi wa haki.

"Ukifuatilia vizuri utabaini kuna baadhi ya halmashauri kuna kesi za PCCB (TAKUKURU) ambazo zipo hatua mbalimbali, pia siku ya uzinduzi wa Mwenge itatolewa taarifa ya tathmini Mwenge ulikopita na huu unaofuata na mambo ya kuzingatiwa, ambapo Mheshimiwa Makamu wa Rais kuna mambo atasema ambayo yatakuwa ni mrejesho wa kile kilichofanyika kwa mwaka uliopita. Kwa hiyo, sitaki nimwingilie Makamu wa Rais katika hilo," alifafanua.

Naibu Waziri Katambi alisema kuwa kwenye halmashauri zilizobainika miradi kuwa na dosari, kesi zake zinaendelea, mojawapo ni Manispaa ya Temeke.



Miundombinu iliyowekwa ili kuzuia watu kukatisha kwenye bustani ya Barabara ya Sam Nujoma, ikiwa imeharibika na kutelekezwa katika eneo la Mwenge, mkoani Dar es Salaam. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Mahakama yatupa rufani ya aliyemuua mume mwenziwe

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA ya Rufani Tanzania Kanda ya Mtwara imetupilia mbali rufani ya Mahamudu Chupa, aliyehukumiwa kunyongwa hadi kufa kwa kumuua mume mwenzake baada ya kuona haina mashiko.

Hukumu ya Mahakama hiyo ilitolewa na jopo la majaji watatu, Jaji Gerald Ndika, Rehema Kerefu na Penterin Kente baada ya kupitia hoja za kupinga adhabu zilizowasilishwa na mrufani kupitia Wakili Robert Dadaya.

Katika hukumu hiyo, mrufani alitiwa hatiani na Mahakama Kuu Kanda ya Mtwara kwa kosa la kuua kwa kukusudia na kuhukumiwa kunyongwa hadi kufa.

Jamhuri katika shauri hilo ilikuwa na mashahidi sita na kwamba mrufani na marehemu Dickson Mnimbo walikuwa wakiishi kijiji kimoja cha Nkowe wilayani Ruangwa mkoani Lindi.

"Hakuna ubishi kwamba marehemu alikuwa akiishi na shahidi wa kwanza, Helena Chitanda baada ya shahidi huyo kuvunja uhusiano wa kimapenzi wa awali kati yake na mrufani," lilisema jopo hilo la majaji.

Inadaiwa kuwa mchana wa Januari Mosi, 2018, mrufani akiwa na rafiki yake aliyetajwa kwa jina la Jirani, walimkuta shahidi wa kwanza akiwa na Mnimbo (marehemu), wakamvamia Mnimbo na kumpiga hadi kusababisha kifo chake.

Inadaiwa kwamba mrufani kufanya kitendo hicho ilikuwa kulipiza kisasi kwa Mnimbo kwa kumchukua aliyekuwa mpenzi wake.

Ripoti ya uchunguzi wa daktari ilionyesha kifo cha Mnimbo kilisababishwa na jeraha kichwani.

Mrufani pamoja na sababu zingine za kupinga adhabu, alidai kwamba jaji hakuchambua vizuri ushahidi wa utetezi na kwamba siku ya tukio, mrufani alifuata vitu vyake kwa shahidi wa kwanza.

Katika utetezi huo, alidai walipigana na Mnimbo na kwamba Jamhuri walishindwa kutoa ushahidi wa kuonyesha jinsi alivyomjeruhi.

Jopo la majaji baada ya kupitia hoja za pande zote mbili, lilisema hakuna ushahidi wa kuonyesha kulikuwa na kupigana kati ya mrufani na Mnimbo.

Mahakama ilikubaliana na hoja za Jamhuri zilizowasilishwa na Wakili wa Serikali Mkuu, Ajuaye Zegeli kwamba rufani itupwe haina mashiko na upande wao walikuwa na ushahidi wa kutosha kuthibitisha kuwa mrufani alitenda tukio hilo.

Jopo la majaji baada ya kusema hayo lilitupilia mbali rufani hiyo kwa sababu haina mashiko kisheria. Mrufani ataendelea kutumikia adhabu aliyopewa.

# Wanafunzi 35 walivyopata ujauzito mwanzo wa mwaka

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WANAFUNZI 35 wa shule za sekondari katika Halmashauri ya Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga wamepata ujauzito katika kipindi cha miezi mitatu ya mwanzoni mwa mwaka, yaani kuanzia Januari hadi Machi mwaka huu.

Kutokana na vitendo hivyo, baadhi ya wahusika wameshaanza kuchukuliwa hatua za kisheria na wengine kesi zao zinaendelea kutajwa mahakamani.

Mjini Kahama jana, Mkaguzi wa Jeshi la Polisi ambaye pia ni Mkuu wa Dawati la Jinsia, Wanawake na Watoto, Tiho Masatu, alibainisha dosari hiyo alipozungumza na waandishi wa habari.

Alisema wameendelea kushirikiana na jamii katika kutokomeza vitendo vya ukatili wa kijinsia hususani kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari.

Masatu alisema idadi hiyo ya wanafunzi waliopata ujauzito katika kipindi hicho kifupi inatisha na inaonyesha ni jinsi gani wazazi na walezi hawana mawasiliano mazuri na walimu wanaowafundisha watoto wao.

Alisema hatua za kisheria zinaendelea kuchukuliwa kwa wote waliohusika kuwasababishia wanafunzi hao ujauzito na kukatisha masomo yao.

Mkaguzi huyo alisema ili kutatua tatizo hilo, ni vyema wazazi kwa kushirikiana na walimu kujenga desturi ya kuzungumza na wanafunzi wa kike na kutatua shida zao.

"Wazazi hatuna budi kubadilisha mitazamo yetu juu ya watoto wetu wa kike, kipindi hiki watoto wanakua na kupevuka mapema na kuingia kwenye matamanio, tujenge desturi ya kukutana na kuzungumza nao juu ya masuala ya uhusiano baina yao na wanaume," alisema Masatu.

Aliongeza kuwa moja ya sababu zinazochangia wanafunzi kuendelea kupata ujauzito shuleni ni kutokana na tamaa za kupata kila kitu, hata ambavyo vipo nje ya uwezo wa maisha yao.



Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Liwale, mkoani Lindi, Mohamed Mtesa (kushoto), akikabidhi baadhi ya mifuko 1200 ya saruji kwa Ofisa Elimu wa Kata ya Liwale Mjini, James Mabula juzi, iliyotolewa na mbunge wa Liwale, Zuberi Kuchauka ili kuboresha miundombinu mbalimbali ikiwamo ya elimu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Rushwa ya ngono yatajwa kikwazo usawa wa kijinsia

**Na Marco Maduhu**

RUSHWA ya ngono imetajwa kuendelea kuwa kikwazo katika kuleta usawa wa kijinsia kwa wanawake kushika nafasi za uongozi.

Mkurugenzi Mwenza wa Mfuko wa Ruzuku wa Wanawake Tanzania (WFT-Trust), Rose Marandu, alibainisha hayo jana mkoani Dar es Salaam, alipofungua mkutano wa mashirika yasiyo ya kiserikali kutoka mikoa mbalimbali, ambayo hupata ruzuku ya kutekeleza miradi ya utetezi wa haki za wanawake na watoto.

Alisema katika ujenzi wa nguvu ya pamoja (TAPO) kwa kupinga masuala ya mfumo dume na kuleta ukombozi wa mwanamke kimapinduzi na kufikia usawa wa kijinsia 50 kwa 50 hasa kwenye nafasi za uongozi, kuna vitu vitatu ambavyo vinapaswa kupingwa ikiwamo rushwa ya ngono.

"Tunashindwa kupata viongozi wanawake kwa sababu ya rushwa ya ngono, inadhalilisha sana na inaumiza. Mfano, kuna mama alimwombea kazi binti yake sehemu fulani, akaombwa rushwa ya ngono na msichana akapata kazi.

"Yule bosi akamwomba na binti yake rushwa hiyo hiyo, akatembea na mama na mtoto, inaumiza sana," Marandu alisema.

Alitaja vitu vingine ambavyo ni kikwazo kwa wanawake kushika nafasi za uongozi kuwa ni pamoja na mila na desturi kandamizi ambazo zimekuwa zikimnyima fursa mwanamke kuwa kiongozi na kutakiwa aendelee kuwa mtu wa kutumikia wanaume na siyo kuwaongoza.

Alisema kikwazo cha tatu ni afya ya uzazi, akifafanua kwamba wanawake wanapopata nafasi za uongozi, hawapati vizuri likizo ya uzazi kwenye baadhi ya taasisi pamoja na kushindwa kunyonyesha vizuri watoto wao kutokana na kupewa majukumu mengi bila kujali kuwa ni wazazi, hivyo kuuona uongozi huo kama kero kwao.

Aliyataka mashirika hayo kuitumia vizuri ruzuku yaliyopatiwa katika kumkomboa mwanamke na kufikia usawa wa kijinsia kwenye nyanja mbalimbali zikiwamo za kiuchumi, kilimo, kumiliki mali na kushika nafasi za uongozi kuanzia ngazi za chini.

Baadhi ya washiriki kwenye mkutano huo walisema kikwazo kikubwa ambacho wamekuwa wakikumbana nacho katika utekelezaji wa majukumu yao ya utetezi wa haki za wanawake na watoto wa kike ni mila na desturi kandamizi ambazo zimeendelea kumkandamiza mwanamke, pia ndoa za utotoni.

# Wanawake wajengewa uwezo uchimbaji madini, mafuta

**Na Romana Mallya**

CHAMA cha Wanasheria Tanganyika (TLS) kwa kushirikisha na Chama cha Wanasheria Canada wamewajengea uwezo wanawake ili kuachana na mila potofu na kujiona wana haki sawa ya kushiriki katika miradi ya uchimbaji wa madini na mafuta.

Mkurugenzi Mtendaji wa TLS, Kaleb Gamaya, ndiye aliyebainisha hatua hiyo jijini Dar es Salaam na kufafanua kuwa mafanikio hayo yamepatikana kupitia Mradi wa SIRD wanaoutekelekeza kwa kushirikiana na Canada ambao unalenga ukuaji endelevu wa uchumi kwa watu wa Afrika Mashariki hususani wanawake na makundi yaliyo katika mazingira magumu yanayoathiriwa na sekta ya uziduaji.

Alisema kupitia mradi huo nchini wameweza kuwafikia wanawake kwa kuwaelimisha umuhimu wao katika shughuli hizo.

"Mapendekezo yetu tumeona wanawake wanahaki sawa ya kushiriki katika miradi ya uchimbaji wa madini na uziduaji. Zipo sheria na kanuni katika ngazi za mitaa hadi serikali kuu ambazo zimehakikisha zimeweka mazingira ya ushiriki wa wanawake katika shughuli hizi.

"Lakini tumebaini zipo tamaduni ndani ya jamii ambazo mwanamke anaonekana akienda migodini eti anafukuza madini yasipatikane kitu ambacho siyo kweli, kupitia mradi huu wa miaka mitatu ambao tumebakiza miezi tisa umalizike tumetoa elimu kwa makundi mbalimbali ili kuongeza ushiriki wa mwanamke ambaye ni mdau mkubwa wa maendeleo."

Gamaya alisema ushiriki wa wanawake katika shughuli hizo ni muhimu lakini kundi hilo limekuwa likiwekwa pembeni kutokana na imani hizo za kitamaduni.

"Leo (jana) tumekutana na wadau mbalimbali wakiwamo watumishi wa umma, wanasheria na wadau wetu wa Canada tunangalia mradi umefanikiwa, je, tumeweka misingi imara? Je, wanawake katika maeneo yao hasa yale yanayozungukwa na migodi wanaweza kujisimamia, kutetea haki zao na za wengine?" Alisema.

Mjumbe wa kamati ya ushauri ya mradi SIRD, Aisha Sinde, alitaja moja ya mafanikio tangu kuanza kwa mradi huo mwaka 2017 ni namna walivyoweza kukuza uelewa ndani ya jamii hususan kwa wanawake katika masuala ya uchimbaji wa mafuta na uziduaji.

Alisema mradi umeielimisha jamii hasa zinazozunguka migodi na maeneo ya uchimbaji mafuta umuhimu wa kuzijua sheria.

Mwenyekiti wa kikundi cha Walagabishi, Christina Gamba, alisema kupitia mradi huo wameweza kujifunza sheria mbalimbali ambazo zimekuwa msaada kwao katika kuelimisha jamii.

"Tumekuwa tukitoa msaada wa kisheria kwa wanawake na watoto katika eneo la ukatili wa kijinsia. Mradi huu umetuwezesha kujifunza zaidi sheria za sekta ya uziduaji (madini, gesi na mafuta) ambazo awali tulikuwa hatuzijui na kusababisha ushiriki wetu katika sekta ya madini na uchimbaji wa mafuta kuwa mdogo," alisema.

HABARI KITAIFA

# Mbunge amwaga saruji mifuko 1,200 ujenzi miundombinu

**Na Sabato Kasika**

MBUNGE wa Liwale mkoani Lindi, Zuberi Kuchauka, amekabidhi mifuko 1,200 ya saruji yenye thamani ya Sh. milioni 19.2 kwa ajili ya uboreshaji wa miundombinu mbalimbali ikiwamo ya elimu na afya jimboni mwake.

Katibu wa mbunge huyo, Jaizu Mkinde, alisema makabidhiano ya saruji hiyo katika maeneo yaliyokusudiwa, yalifanyika mwanzoni mwa wiki, na kumalizika juzi.

"Mbunge ametoa mifuko 200 ya saruji katika gereza la Wilaya ya Liwale, ametoa mifuko mingine 200 kwa Shule ya Msingi Tuungane, mingine 100 kwa Shule ya Msingi Mtwango," alisema Mkinde.

Mingine 100 imetolewa ili kujenga hosteli ya wasichana wa Shule ya Sekondari Nangano, mifuko 100 katika Shule ya Sekondari Kibutuka na mingine 100 kwa Shule ya Msingi Kuchochorokana.

"Shule ya Msingi Naluleo imepata mifuko 100, Darajani Day Care mifuko 100, Kiangaro Sekondari mifuko 100, zahanati ya Kijiji cha Ngorongopa mifuko 100 na Kituo cha Afya Kata ya Barikiwa mifuko 100," alisema.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Liwale, Mohamed Mtesa, alisema halmashauri yake ina shule za msingi 55 na kwamba kuna upungufu wa madarasa 10 na wako mbioni kukamilisha ujenzi wa nadarasa matano.

"Tumetenga Sh. milioni 200 katika bajeti yetu ya mwaka 2022/2023 kwa ajili ya kujenga madarasa 10, tunakaribia kumaliza matano na tutaendelea kukamilisha ujenzi mengine," alisema Mtesa.

Mtesa aliwaomba wadau wa maendeleo wa ndani na nje ya Liwale, kuendelea kuunga mkono juhudi za halmashauri hiyo katika uboreshaji wa miundombinu mbalimbali ikiwamo ya elimu na afya.

"Mbunge Zuberi Kuchauka, ni miongoni mwa wadau wakubwa wa maendeleo ya wilaya ya Liwale, lakini ninawaomba wadau wengine kuungana naye katika juhudi za kuboresha huduma mbalimbali wilayani mwetu," alisema.

Alisema, mbali na mifuko hiyo 1,200 ya saruji, amekabidhi pikipiki tano kwa vijana wa kikundi cha madereva wa bodaboda wa mjini Liwale ili ziwasaidie katika biashara yao ya usafirishaji wa abiria.

"Halmashauri yetu inamshukuru kwa jitihada zake anazofanya kwa ajili ya maendeleo ya Liwale na wananchi wake kwa ujumla," alisema.

# Mabula afunguka ushawishi ugawaji ardhi kwa wawekezaji

**Na Munir Shemweta,** WANMM DODOMA

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, ametaka elimu ya kuwatahadharisha wananchi kuhusu kujiepusha na vishawishi visivyo na tija vinavyosababisha ugawaji maeneo ya ardhi kwa ajili ya uwekezaj kwa kupewa ahadi zisizotekelezeka.

Dk. Mabula alisema hayo wakati akifungua kikao kazi cha wadau wa Uandaaji, Usimamizi na Utekelezaji wa Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi nchini kilichofanyika jijini Dodoma.

"Tunategemea ninyi wadau mnakuwa sehemu ya kuelimisha wananchi kutambua thamani ya ardhi na kutokuwa wepesi kuachia ardhi kwa sababu ya tamaa ya wawekezaji, wanakuja halafu wanakupa ahadi isiyotekelezeka, na mwisho wa siku wananchi wanapeleka kilio serikalini," alisema.

Kwa mujibu wa waziri huyo, elimu itakayotolewa itakuwa ni kwa ajili ya kuwafungua akili wananchi hasa wale wa vijijini kutokuwa na wasiwasi na tamaa ya kupokea vishawishi ambavyo mwisho wa siku havitekelezi.

"Kuna maeneo watu wa Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi wamepanga na mwekezaji anaahidi kitu ambacho hakitekelezeki na wananchi wanakuwa na tamaa kuwa watajengewa shule, zahanati au kuchimbiwa kisima na mwekezaji ataanza mchakato kidogo kidogo, lakini mwisho wa siku hakuna kinachofanyika na wakati huo ardhi ishachukuliwa na migogoro inakuwa mingi hivyo tusingependa haya yajirudie," alisema Mabula.

Ameitaka Tume ya Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi nchini kwa kushirikiana na wadau kuongeza kasi ya uelimishaji wananchi kuhusu uandaaji na utekelezaji mipango ya matumizi ardhi ili mipango hiyo inapoidhinishwa na mamlaka husika basi iweze kutekelezwa na kusimamiwa kwa umakini.

Katibu Mkuu Wizara hiyo, Dk. Allan Kijazi, aliwataka washiriki wa kikao hicho cha wadau kuja na mikakati itakayoishauri Tume ya Matumizi ya Ardhi namna bora itakayosaidia uwepo wa vipaumbele katika kuchagua maeneo ya kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi.

"Tanzania tunavyo vijiji visivyopungua 14,000 na kati ya hivyo takriban vijiji 2,000 ndivyo vyenye mipango ya matumizi bora ya ardhi, hivyo bado tunayo kazi kubwa ya kufanya ili kuongeza kasi na lazima kujiuliza tunaanzia wapi," alisema Dk. Kijazi.

Mkurugenzi wa Idara ya Maendeleo ya Makazi Wizara, Deogratius Kalimenze, aliwataka wadau kuhakikisha kazi wanazozifanya na kukamilisha kwenye mamlaka ya serikali za mitaa taarifa zake zinawasilishwa kwa wakati ili kufanyiwa kazi na tume na waziri aweze kutangaza gazeti la serikali na kusisitiza kuwa mipango yote iliyokamilika lazima itangazwe kwa wakati.



Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Liberata Mulamula (kushoto), akizungumza kwenye kongamano la 'Women Lead Forum' lililoandaliwa na Taasisi ya Southern Africa Embrace, jijini Dar es Salaam juzi, lililolenga kuhamasisha viongozi wanawake katika jamii ili kuleta mafanikio endelevu ya kiuchumi na kujenga usawa wa jinsia. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mtwara yapewa mbinu kufuta sifuri

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

UMOJA wa maofisa elimu kata mkoa wa Mtwara umehimizwa kufanya kazi kwa bidii na kujituma ili kuleta matokeo chanya ya ufaulu wa juu kwa wanafunzi na kufuta daraja sifuri kwenye maeneo yao. Ushauri huo ulitolewa jana wilayani Masasi mkoani Mtwara na Ofisa Elimu wa Mkoa wa Mtwara, Kiduma Mageni, alipokuwa akizungumza na maofisa 151 wa mkoa wa Mtwara kwenye kikao cha umoja wa maofisa elimu kata, kikao kilichofanyika mjini hapo.

Alisema sekta ya elimu katika mkoa huo imejikewea malengo saba katika kuhakikisha wanainua kiwango cha elimu katika mkoa huo.

Mageni alisema malengo hayo saba ni mahususi kwa ajili ya kuona kila mmoja anafanya kazi kwa bidii na kwa moyo ili hali ya ufaulu ipande na kuufanya mkoa kuondoka katika sifa ya kutofanya vizuri kielimu, kulinganisha na mikoa mingine.

Alisema maofisa elimu kata ni nyenzo muhimu katika sekta ya elimu, hivyo iwapo wakisimamia vyema shughuli za kielimu kwenye maeneo yao, hali ya ufaulu itapanda kuwa katika kiwango kizuri na kuufanya mkoa huo kuwa na sifa bora ukilinganisha na miaka ya nyuma.

"Twendeni tukafanye kazi kwa nguvu kubwa na uweledi wetu wote sisi maofisa elimu kata tukifanya kazi kwa kushirikiana sote kwa pamoja ...hii habari ya kuwa na wanafunzi wasiojua kusoma na kuandika na wengine kupata daraja sifuri kwenye mitahani yao haitakuwapo tena," alisema Mageni.

Awali akifungua mkutano huo, Mkuu wa Wilaya ya Masasi, Claudia Kitta, alisema maofisa elimu kata wanapaswa kujitambua katika kutimiza wajibu wao, kwani wao ndio chachu ya maendeleo katika sekta ya elimu.

"Inasikitisha sana kuona katika mkoa wa wetu kuna baadhi ya wanafunzi kwenye baadhi ya shule anafika darasa saba na hajui kusoma na kuandika na katika mitihani ya kitaifa kusababisha kupata daraja sifuri...hii twende sasa tukafanye kazi kwa uweledi na bidii ili matatizo haya yasiwapo," alisema Kitta.

HABARI KITAIFA

# Wasomi Chuo cha Mzumbe walivyomlilia Prof. Ngowi

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

WAHADHIRI wa Chuo Kikuu Mzumbe mkoani Morogoro wameeleza kupokea kwa mshtuko mkubwa kifo cha mhadhiri na mfanyakazi mwenzao wa uchumi, ambaye ni Mkuu wa Ndaki ya Dar es Salaam, Prof. Honest Ngowi aliyefariki kwa ajali ya barabarani.

Alikufa baada ya gari lake kuangukiwa na kontena kwenye ajali iliyohusisha magari matatu katika eneo la Mlandizi mkoani Pwani.

Nipashe ilifika chuoni hapo na kukuta hali ya simanzi kutokana na kifo cha Prof. Ngowi na dereva wake, Innocent Mringo.

"Taarifa hizi tumezipokea kwa masikitiko makubwa sana, kwa niaba ya makamu mkuu wa chuo na uongozi mzima, tunatoa pole sana kwa familia ya Prof. Ngowi, ndugu, jamaa na marafiki kutokana na msiba huu wa ghafla," alisema Rose Joseph, Mkurugenzi wa Mawasiliano wa Chuo Kikuu Mzumbe.

Alisema alikuwa maarufu kutokana na namna alivyokuwa akiitumia taaluma yake, ambayo hakuitumia kwa manufaa ya chuo hicho pekee, bali kwa jamii kwa ujumla ikiwamo kutoa mafunzo kwa umma kwenye makongamano, semina za ndani na nje ya nchi, hivyo kuwa mwakilishi mzuri wa chuo hicho.

Prof. Ernest Kihanga alisema anamkumbuka Prof. Ngowi tangu akiwa mwanafunzi mwenzake IDM Mzumbe, akimtangulia darasa moja, na kuanza wote kazi Mzumbe, Ngowi akianza 1995 na yeye 1996, baadaye kwenda wote masomoni Norway kuchukua Shahada ya Uzamili, hivyo alimfahamu vizuri sana.

"Nimemfahamu pia nikiwa kama kiongozi wake, wakati huo nikiwa Naibu Makamu Mkuu wa Chuo nashughulikia Utawala na Fedha, kipindi hicho alichaguliwa kuwa Mkuu wa Ndaki ya Dar es Salaam na nilifanya naye kazi vizuri sana... alikuwa na uwezo mzuri wa kufanya kazi, hata kampasi ya Dar es Salaam aliiongoza vizuri sana ikapiga hatua kubwa ya kujivunia," alisema Prof. Kihanga.

Akasema wanajumuiya wa Chuo Kikuu Mzumbe wamepata pigo kubwa sana, kwani wamefanya naye kazi kwa muda mrefu na waliufahamu uwezo wake, mchango wake ulikuwa mkubwa sana katika masuala ya uchumi, ujasiriamali na mtu aliyekuwa haoni tabu kujitolea bila malipo kufundisha jamii kupitia mihadhara mbalimbali.

"Tumepata pigo kubwa kwa nchi na kwa jamii, alikuwa bado ni profesa mdogo, lakini Mungu amempenda zaidi, mimi nilipokea taarifa hizi kutoka kwenye mitandao ya kijamii, nilistuka sana, sikuamini, nilipoona zinazidi kusambaa nikampigia rafiki yangu kujiridhisha, na baadaye nilipoona taarifa ITV ndio nikaamini, kwa kweli ni pigo kubwa sana," aliongeza Prof. Kihanga.

Mhadhiri mwingine Dk. Arbogast Musabila alisema Prof. Ngowi alikuwa ni kumbukumbu ya taasisi ya Mzumbe kutokana na kusoma tangu chuo hicho kikiwa IDM na aliwaunganisha wadau wengi na chuo hicho wa ndani na nje ya nchi.

"Nikimtizama kama baba wa familia, ni baba aliyekuwa na maono, aliyesimamia familia yake na hata mafanikio ya watoto wake kwake ilikuwa kitu cha muhimu, kama chuo tumepoteza sana, alikuwa ni suluhisho la mambo mengi, kuanzia ufundishaji wake, alivyokuwa akifanya kazi za ushauri, utafiti lakini taasisi nyingi alizofanyia kazi.

"Alichukua taswira ya chuo na hakika pengo lake litachukua muda mrefu, hasa wakati huu ambao alikuwa akikitizama Chuo Kikuu Mzumbe kwenda kwenye mapinduzi ya viwanda ya kidijitali na matumizi ya kiteknolojia katika uchumi," alisema Dk. Musabila.




Mkurugenzi wa Vodacom M-Pesa, Epimack Mbeteni (kushoto), akizungumza na maofisa kutoka Benki Kuu ya Ethiopia na kampuni ya simu za mkononi ya Safaricom Ethiopia, kuhusu huduma za kifedha kwa njia ya mtandao zinavyoleta tija kwa jamii na kuongeza pato la taifa kwa kufuata sheria na mamlaka husika za nchi, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Ujumbe huo umekuja nchini kwa lengo la kujifunza huduma jumuishi za kifedha kwa njia ya mtandao wa simu za mkononi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Makundi maalum Masasi yaonyeshwa fursa mikopo

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

WANAWAKE, vijana na watu wenye ulemavu wa Halmashauri ya Mji wa Masasi mkoani Mtwara, wamesisitizwa kujitokeza kwa wingi na kuendelea kuunda vikundi vya ujasiriamali ili kupatiwa mikopo.

Imeelezwa kwamba halmashauri katika mwaka ujao wa fedha 2022/2023 imekusudia kutoa zaidi ya Sh. milioni 129 kwa vikundi hivyo vya ujasiriamali.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Masasi, Eliasi Ntiruhungwa, ndiye aliyetoa msisitizo huo alipokuwa akizungumza na gazeti hili, juu ya mikakati mbalimbali ya halmashauri katika mwaka ujao wa fedha.

Ntiruhungwa alisema moja ya mikakati iliyojiwekea halmashauri katika kuinua uchumi kwa wananchi wake hasa wa chini, ni kuendelea kutoa mikopo inayotokana na mapato ya ndani ambayo ni asilimia 10 kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu, lengo likiwa kundi hilo liweze kujikwamua na umaskini wa kipato.

Alisema kuwa katika mwaka wa fedha uliopita, vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu vilifanya vizuri katika marejesho ya fedha walizokopeshwa na halmashauri, hivyo wasisite kuendelea kuunda vikundi ili kuendelea kukopeshwa mikopo zaidi.

Alisema halmashauri hiyo wiki iliyopita ilitoa zaidi ya shilingi milioni 60 kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu na kwamba wiki ijayo halmashauri inajipanga kutoa zaidi ya shilingi milioni 40, hivyo makundi hayo ni fursa kwao kutumia fedha hizo kwa malengo yaliyokusudiwa ili kujikwamua dhidi ya umaskini.

Ntiruhungwa alisema kwamba katika mwaka ujao wa fedha halmashauri imetenga zaidi ya shilingi milioni 129 kwa ajili ya kukopesha vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

## Kesi wizi fedha za msikiti kuanza kusikilizwa Aprili 20

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu inatarajia kuanza usikilizaji wa awali wa shauri dhidi ya Akshary Motichand na wenzake watatu wanaotuhumiwa kula njama na kuiba zaidi ya Sh. milioni 480, mali ya Msikiti wa Shree Sanatan, Dharma Sabha Aprili 20, mwaka huu.

Uamuzi huo ulitolewa jana mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi Godfrey Issaya baada ya Wakili wa Serikali, Grace Mwanga kuomba kuahirisha kesi.

Wakili Mwanga alidai upelelezi wa kesi hiyo ulishakamilika, hivyo wanaomba tarehe nyingine ya kuanza usikilizwaji wa awali (PH) kwa kuwa wanataka kufanya marekebisho katika hati ya mashtaka.

Mahakama ilikubali maombi hayo na kuahirisha kesi hadi Aprili 20, mwaka huu kwa ajili ya PH.

Washtakiwa katika kesi hiyo ni Motichand (22), Vasant Solanki (73) na Ramesh Shah (62).

Inadaiwa katika shtaka la kwanza kuwa, washtakiwa wote kwa pamoja kati ya Januari 2016 na Novemba 2016, jijini Dar es Salaam, walikula njama ya kuiba.

Katika shtaka la pili, Akshary anadaiwa katika kipindi hicho, jijini Dar es Salaam, aliiba Sh. milioni 480.509, mali ya Msikiti wa Shree Sanatan, Dharma Sabha.

Washtakiwa walikana kutenda makosa hayo na mahakama ilikubali kuwapa dhamana kwa masharti ya kuwa na wadhamini wawili, wawasilishe fedha taslimu Sh. milioni 60 au hati ya mali isiyohamishika.

Washtakiwa walifanikiwa kupata hati za mali isiyohamishika na wote wako nje kwa dhamana.




Ukurasa 12

**Talaka inavyochangia mstari wa maisha na ndoa kupasuka Z'bar**



Ukurasa 13

Misuguano Ikulu ya Kenya kumpatia ushindi Raila Odinga uchaguzi 2022?



Ukurasa 14

**MADELEINE ALBRIGHT**

**Mwanamke wa shoka anayekumbukwa kwa misimamo yake ya kidiplomasia**

siasa
JUMATANO MACHI 30, 2022
HABARI BORA NA KAMILIFU
Nipashe

# Msekwa anapoungana na maelekezo ya Rais Samia kuhusu nini kifanyike

• Sakaya: Sisi CUF tuna angalizo letu

**Na Sabato Kasika**

IKIWA leo ni siku ya 11 tangu Rais Samia Suluhu Hassan, aanze mwaka wa pili katika nafasi hiyo, imeelezwa uongozi wake unaonyesha mwanga wa kujenga daraja la kuaminiana kati ya serikali na vyama vya upinzani.

Mwanasiasa mkongwe nchini, Pius Msekwa, ambaye ameshika nafasi mbalimbali za uongozi ndani ya CCM na serikalini, anasema aina hiyo ya uamuzi inaondoa lawama na manung'uniko kwa vyama vya vingine, ambavyo huko nyuma vilikosa nafasi.

Akihojiwa na shirika moja la habari kuhusu Mwaka Mmoja wa Rais Samia Suluhu Hassan, Msekwa anasema mtindo huo wa uongozi ni wa kipekee na unaimarisha demokrasia.

"Staili yake imeonyesha wazi kwamba anataka kufanya mambo yake kwa mujibu wa misingi ya demokrasia iliyomo ndani ya katiba, kwa maana ya kutoa nafasi kwa watu kushiriki kutoa mawazo yao," anasema Msekwa, aliyewahi kuwa Spika wa Jamhuri ya Muugano.

Anasema, Rais Samia amekuwa na shauku ya kuona watu wanashiriki kuchagua viongozi wao kwa uhuru na kuhakikisha kila kitu kinaegemea kwenye katiba.

"Ninamsifu kwa hilo kwamba mtindo wake kwa upande huo wa siasa umeonyesha ana nia ya kujenga daraja kati yake na kambi ya upinzani ili kujenga taifa moja linaloshirikiana katika maendeleo ya nchi," anasema.



Mzee Pius Msekwa. **PICHA: MTANDAO**

**MAONO YA VYAMA**

Makamu Mwenyekiti Bara wa Chama cha Alliance for African Farmers Party (AAFP), Nancy Mrikaria, anasifu kuwa uhai wa vyama vya saiasa umerudi tena na kuashiria mwanzo bora.

"Wengine hatukupata nafasi ya kuzungumzia kabla ya mwaka mmoja, lakini niseme kuwa ameonyesha dalili za kuweka mazingira mazuri ya kuimarisha demokrasia ndani ya vyama," anasema Mrikaria.

Anasema rais anaendelea kuweka mazingira rafiki, akitoa mfano hatua alizochukua wakati akipokea mapendekezo ya wadau wa demokrasia ya vyama vingi vya siasa.

"Rais ameagiza kufanyiwa maboresho yote yaliyomo katika mapendekezo ya kikosi kazi kilichomkabidhi mapendekezo hayo, kwamba kiangalie haja ya kurekebisha katiba iliopo," anasema.

Mwanasiasa huyo anatoa imani yake kwamba, Rais Samia anataka kurekebisha baadhi ya maeneo yanayolalamikiwa na hata kama kutakuwa na haja ya kuandika katiba mpya, basi kazi kubwa itakuwa imeshafanywa kwenye maboresho hayo.

"Mchakato wa katiba mpya unatumia fedha nyingi, hivyo kitendo cha Rais kutoa maagizo hayo, kinalenga pia kuokoa fedha za walipa kodi. Ninaamini kuwa iwapo maboresho yatafanyika kikamilifu, malalamiko katika uchaguzi yanaweza kuisha," anasisitiza.

Naibu Katibu Mkuu wa CUF Bara, Magdalena Sakaya, anasema vipo baadhi ya vipengele katika katiba ambavyo wadau wa siasa wamekuwa wakivilalamikia na anatamani virekebishwe kabla ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa 2024.

"Hitaji la wadau wa demokrasia ni katiba mpya, lakini kama kuna changamoto za kuipata kwa wakati, si vibaya kuifanyia marekebisho iliyopo kabla ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa Mwaka 2024,"anasema Sakaya.

Anataja kikwazo kimojwapo ni kukabiliana na Jeshi la Polisi wanaoingilia mikutano yao vyama vya siasa, sasa anataka sheria ya kuwazuia wasiendelee kusababisha mtafaruku katika siasa.

"Kwa kuwa ni wazi kuwa kupata katiba mpya kwa sasa ni vigumu, yawekwe mazingira mapya ya demokrasia, katika siasa na uchaguzi kwa kurekebisha vipengele vyote vinavyolalamikiwa kwenye katiba ya sasa," anasema.

Anashauri kwamba marekebisho hayo yanapofanyika, yakiwamo yanayohusu tume huru ya uchaguzi inayokubalika kwa wadau wote, akiamini uchaguzi utakuwa huru na haki na kuondoa malalamiko yanayojitokeza kwenye kila uchaguzi.

"Pia, suala la wagombea kupita bila kupingwa ni tatizo kubwa ambalo hujirudia kila uchaguzi na linatokana na mbinu chafu za kisiasa zinazofanywa na watu," anasema, akihimiza nalo ni muhimu likarekebishwa.

Sakaya anarejea Uchaguzi wa Serikali za Mitaa 2019, wagombea wengi wa upinzani walienguliwa bila sababu zisizo na mashiko na hata kufanya wapinzani wao kutoka chama tawala kupita bila ya kupingwa.

" Raha ya ushindi ni kupambana, na si ushindi wa mezani ambao baadhi ya wanasiasa wamekuwa wakiupata, hivyo sheria zirekebishwe ili mgombea asipite bila kupingwa," anasisitiza.

PENGO LA UTAWALA BORA

# Talaka inavyochangia mstari wa maisha na ndoa kupasuka Z'bar

• Penye sheria, imani wakiri 'shida iko' • Chozi la wazi watoto kukoseshwa shule



Maharusi watarajiwa (waliosimama nyuma), baada ya kukabidhiwa vyeti vya mafunzo ya ndoa ya miezi mitatu, Unguja. **PICHA: MAKTABA**

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

INAPOANGALIWA dhana utawala bora, ujumbe wake mkuu unaangukia utendaji haki kwa pande zote za jamii.

Utawala bora unaanzia katika mifumo ya utawala na kisha inaangukia mustakabali wa kijamii, ikiwamo mifumo mbalimbali ya uhusiano, hapo ikiangukia dhana mojawapo ya ndoa.

Ni kwa bahati mbaya, eneo hilo linapwaya katika utawala bora, kukiwapo misuguano mingi na inaishia katika athari kwa familia, waathirika wa kwanza ni watoto.

Kadhi wa Mahakama ya Wilaya ya Kaskazini 'B', Sheikh Mohammed Ramadhani Khamis, anasema chanzo kikuu cha ongezeko la talaka ni uelewa mdogo wa elimu ya ndoa kwa jamii.

"Ndoa za zamani zilidumu kwa sababu wanandoa walivumiliana na walithamini ndoa zao tofauti na sasa, wanandoa hawana maelewano na wanashindwa kuvumilia changamoto za ndoa," anasema.

Sheikh Mohammed, anasema matatizo mengi yanayosababisha ndoa kuvunjika yanachangiwa na wanaume kushindwa kutimiza majukumu yao, wakiwaachia wanawake mzigo wa kulea familia, nao wanaelemewa na wanashindwa kumudu mahitaji muhimu, watoto wanasitishiwa masomo.

Ofisa wa Dawati la Jinsia Polisi Mkoa wa Kaskazini, Koplo Thabit Makame, anataja chanzo kingine cha kuongezeka talaka ni ndoa nyingi kufungwa katika umri mdogo, wengi katika umri chini ya miaka 25.

Msaidizi Sheria Wilaya ya Kaskazini B, Omar Ali Khamis, anataja udhalilishaji nao unachangia kuongezeka talaka, kwa sababu badala ya kesi kufikishwa mahakamani, familia mbili zinaamua kuwaozesha watoto wao wakati hawako tayari kuingia katika uhusiano.

> "Wanandoa wanapoachana mzigo wa malezi huachiwa mama, kwa hiyo ufuatiliaji wa watoto huwa mdogo kwa sababu mama anakuwa na majukumu mengi.

Askofu wa Kanisa la Anglikana Zanzibar, Michael Hafidh, anasema wanandoa kutokuwa na hofu ya Mungu imechangia ndoa nyingi kuvunjika.

Mwanaharakati anayetetea haki za wanawake na watoto Mkoa wa Kaskazini Unguja, Hadia Ali, anahusisha ukuaji teknolojia na hasa simu za mkononi na ongezeko la talaka, kwa sababu wanandoa wanashindwa kuaminiana.

"Alikuwa hatulii nyumbani na nilipomkanya alikuwa ananitishia amani, mara nyingine alijaribu kutaka kuniua wakati nimelala, nimeamua nimpe talaka ili kila mmoja awe na maisha yake," anasema Juma Ali, mkazi wa kijiji cha Mkokotoni Wilaya ya Kaskazini Unguja.

### SURA YA TALAKA

Mama Siwema Khamis (45), ana simulizi ya yaliyomkuta, akifafanua sababu zinazochangia talaka yake: "Niliolewa na wanaume wanne tofauti, lakini wote wameniacha na kunitupia mzigo wa kulea watoto huku wengine wakikatisha masomo,"

Siwema, mwenye watoto watano mkazi wa kijiji cha Donge Mkoa wa Kaskazini Unguja, anasimulia madhila anayopitia kulea watoto bila msaada wa baba yao, huku binafsi akiwa hana ajira ya kumuingizia kipato.

Anasema vyanzo vya kuvunjika ndoa zake vinafanana; kutelekezwa na waume zake, baadhi ya watoto kushindwa kuendelea na masomo na mwingine kubeba ujauzito akiwa na umri mdogo.

"Kati ya watoto wangu watano, mtoto wangu wa mwanzo wa kiume ameshindwa kuendelea na masomo kwa sababu sina uwezo na sina msaada wa kupata huduma kutoka popote, wa pili amebeba ujauzito akiwa na umri mdogo," anaeleza.

Anataja shida anazopitia, ni miongoni mwa matatizo mengi wanayopitia wanawake na watoto wengi wa Zanzibar baada ya ndoa zao kuvunjika.

Kadhi wa Mahakama ya Wilaya Kaskazini 'A' Unguja, Omar Shehe Khamis, anasema kwa kawaida ndoa zinapovunjika, mama hubeba mizigo na watoto wake kurudi nyumbani. Pia, tatizo la kukatishwa masomo huibuka.

"Wanandoa wanapoachana mzigo wa malezi huachiwa mama, kwa hiyo ufuatiliaji wa watoto huwa mdogo kwa sababu mama anakuwa na majukumu mengi," anasema Khamis.

Anataja lingine ni uelewa mdogo, kutokujua kusoma na kuandika katika baadhi ya mikoa (anataja), hivyo wazazi wanakosa mwamko wa kupeleka watoto shule.

"Ni jambo la kawaida kuwakuta watoto wawili hadi watatu wenye umri wa kwenda shule katika kaya moja wapo nje ya mfumo wa elimu bila sababu ya msingi, sasa tatizo linakuwa kubwa wanandoa wanapoachana," anasema.

### WAATHIRIKA

Asha Hamad (13) sio jina lake halisi, anayeishi kijijini Fukuchani mkoa wa Kaskazini Unguja, ameshindwa kuendelea na masomo baada ya wazazi wake kutalakiana.

"Wazazi wangu waliachana nikiwa darasa la sita. Niliondoka na mama kwenda kuishi nyumbani kwao Mahonda, lakini nilishindwa kuendelea na masomo kwa sababu mama hakuwa na uwezo wa kununua vifaa vya shule," anasema Asha.

Asha ni miongoni mwa wanafunzi walioacha shule kutokana na wazazi kutalakiana, hivyo wanakosa uangalizi wa karibu wanapokuwa shuleni na nyumbani.

Kwa mujibu wa takwimu kutoka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, watoto 6,477 walio na umri wa kwenda shule wapo nje ya mfumo mkoani Kaskazini Unguja.

Watoto hao ni sawa na asilimia 18.5 ya watoto 35,000 walio nje ya shule Zanzibar, kwa sababu mbalimbali ikiwamo utoro, mimba, kuishi katika mazingira magumu na umaskini.

Wengi wao sasa wamejiingiza katika ajira za utotoni katika sekta ya uvuvi, ufugaji na biashara. Idadi hiyo ya watoto walio nje ya mfumo wa elimu, hujumuisha wanafunzi wa shule za msingi na sekondari na wengine hawakuandikishwa kwenda shule au kuishia njiani.

Sera ya Elimu ya Zanzibar ya mwaka 2006, inaelekeza kila mtoto aliyefikia umri wa kwenda shule kuandikishwa ili kunufaika na haki ya elimu bila kikwazo.

### UMASIKINI

Mwakilishi wa Viti Maalum katika Baraza la Wawakilishi Mkoa wa Kaskazini Unguja, Mwajuma Kassim, anasema wakazi wengi wanaishi chini ya kipato Dola ya Marekani moja (Sh.2,300) kwa siku, ukiwa chini ya mstari wa umaskini.

"Licha ya kwamba elimu inatolewa bila malipo, lakini mzazi anatakiwa kugharamia baadhi ya vifaa vya shule kama madaftari na sare, hivyo kwa wazazi maskini kama hawa inakuwa vigumu kumudu," anasema Mwajuma.

Anasema sababu ya umasikini, watoto wanaenda shule wakiwa na njaa, hivyo wanashindwa kuelekeza akili zao katika masomo na hatimaye wanaamua kutoroka.

INAENDELEA UK. 13

# Misuguano Ikulu ya Kenya kumpatia ushindi Raila Odinga uchaguzi 2022?

**Na Moshi Lusonzo**

RAIS Uhuru Kenyatta wa Kenya, amezidisha joto la uchaguzi mkuu baada ya kumtuhumu naibu wake, William Ruto, alikuwa na mpango wa kuipindua serikali yake.

Kauli ya kiongozi huyo ameitoa siku chache akiwa na wazee wa kabila la Kikuyu, akidai Ruto ana tamaa ya madaraka kiasi ambacho alisuka njama ya kuhujumu serikali yake ili aondolewe madarakani.

Kauli kama hizo zimekuwa za kawaida kati ya Rais Kenyatta na naibu wake Ruto, kiasi ambacho huwezi kuamini kama wawili hao walikuwa marafiki wakati wakiingia madarakani kwa mwamvuli wa chama cha Jubilee.

Hata hivyo, Ruto akiwa kaunti ya Mombasa, amekana tuhuma hizo na kueleza kwamba yeye ndiye amewezesha Kenyatta kuingia madarakani.

Anasema anashangazwa na madai kama hayo yanatolewa na kiongozi aliyekabidhiwa Ikulu na kukemea kwamba inaweza kuleta vurugu na mgawanyiko.

"Mimi nilisaidia Uhuru Kenyata kuingia madarakani, naweza kupindua mtu niliyemsaidia? hatutaki misingi ya kikabila tulimchagua aache maneno" Ruto aliwaambia wafuasi wake.

Tangu mkutano wa kwanza kati ya rais Uhuru Kenyatta na mpinzani wake Raila Odinga uliolenga kuleta amani nchini humo uliofanyika Machi 2018, Ruto ameonekana kuwa mbali katika maamuzi muhimu ya serikali huku vyanzo vilivyo karibu na wawili hao vikisema kwamba Ruto ameonekana kufadhaishwa zaidi.

Mzozo wa viongozi hao unaonekana kumuathiri zaidi Ruto kutokana na milolongo ya kumzuia kushiriki shughuli za kiserikali na kumuandama kila kukicha.

Wakati wa uzinduzi wa ripoti ya BBI katika ukumbi wa Bomas of Kenya Novemba 2019, William Ruto, alizuiliwa katika mkutano kati ya rais Uhuru Kenyatta na Raila , pia ilidaiwa kwamba msafara wa magari ya Ruto ulitakiwa kuondoka katika eneo hilo, baada ya Uhuru na Raila kuondoka.

Hivi majuzi Ruto alizuiliwa kusafiri kwenda Uganda akiandamana na muwekezaji mmoja wa Uturuki, ambaye serikali inadai ni mfadhili wa Ugaidi.

Mikutano ya kisiasa ambayo William Ruto alitarajiwa kuhudhuria pia ilifutwa katika dakika za mwisho na mara nyingine polisi wametumia mbomu ya machozi kuwatawanya wafuasi wake.

Aidha wakati wa sherehe za siku ya madaraka iliyofanyika mjini Kisumu , Rais alivunja itifaki ambayo imekuwepo kwa kumualika Raila Odinga na wazungumzaji wengine na kumuacha naibu wake wa rais.



Raila Odinga; Mgombea urais Kenya. **PICHA: MTANDAO**

### MIZOZO INATAWALA IKULU YA KENYA

Imekuwa jambo la kawaida kwa mizozo kutawala Ikulu ya Kenya, kwani mwaka 1966 kulibuka mgogoro kati ya Rais wa kwanza wa taifa hilo mzee Jomo Kenyatta na makamu wake wa rais, Jaramogi Odinga.

Mzee Odinga alihudumu kama makamu wa rais kwa miaka miwili pekee kuanzia mwaka 1964 hadi 1966, alipoamua kujiuzulu baada ya kutengwa na Rais Kenyatta. Katika barua yake ya kujiuzulu ya tarehe 14 mwezi Aprili 1966, Mzee Odinga alisema kwamba Rais Kenyatta alikataa kumtambua kuwa makamu wake katika masuala ya serikali.

Baada ya kuandika barua hiyo pia alistaafu katika chama cha KANU. Alianzisha chama cha upinzani kilichojulikana kama Kenya Peoples Union KPU ambacho kilipigwa marufuku 1969 baada ya vurugu zilizotokea Kisumu , wakati Rais Kenyatta alipozuru eneo hilo ili kufungua Hospitali ya Mkoa ya New Nyanza .

Hata hivyo watoto wa viongozi hao wamefanikiwa kuvunja uadui huo, sasa wamekuwa marafiki kiasi ambacho wanasaidiana katika kuwania uongozi huo wa nchi.

> "Kuungwa mkono na Rais Kenyatta si kwamba nitakuwa chini ya mtu, ananiunga mkono kutokana na malengo yangu ya kuingia Ikulu na si vingine.

### RAILA ANUFAIKA NA MGOGORO

Tangu kutolewa kwa uamuzi wa mahakama ya rufaa kuhusu mradi wa BBI ulioanzishwa na rais Uhuru Kenyatta na ndugu yake Raila Odinga, uhasama kati ya rais na naibu wake umeongezeka na kufikia kiwango ambacho hakijawahi kuonekana awali.

Rais Kenyatta amejitokeza waziwazi kuonyesha mshikamano wake na muungano wa Azimio la Umoja ambao mgombea wake wa urais ni Raila Odinga.

Odinga anapambana na Ruto katika kuwania urais katika uchaguzi Mkuu wa Agosti mwaka huu. Uhuru Kenyatta amekuwa akitofautiana na naibu wake William Ruto, kuhusu uongozi wa taifa hilo kuzunguka kati ya watu wa makabila mawili , ambayo yanatoka mkoa wa kati na Bonde la Ufa.

Odinga ambaye anatoka Magharibi mwa Kenya, ananufaika na mgogoro huo kuwa na uhakika wa kupata uongozi hasa kuungwa mkono na makabila matatu makubwa nchini humo.

Hata hivyo, Odinga alinukuliwa na chombo kimoja cha habari akisema kwamba kamwe hatakuwa kibaraka wa mtu mwingine kama akipewa nafasi hiyo.

Anasema lengo lake ni kwenda Ikulu kudhibiti wezi na mafisadi ambao ndio wanairudisha nyuma Kenya kimaendeleo.

"Kuungwa mkono na Rais Kenyatta si kwamba nitakuwa chini ya mtu, ananiunga mkono kutokana na malengo yangu ya kuingia Ikulu na si vingine," anasema Odinga.

Mzozo kati ya viongozi hao wawili umeathiri utendaji kazi wa ofisi ya wafanyakazi wa umma , idara ambayo inatakiwa kutokuwa na upande wowote ili kuwapatia huduma Wakenya wote.

Wanashindwa kufanya kazi ipasavyo kwa kuhofia kuonekana kama wafuasi wa Ruto , huku maofisa wakuu wa idara hiyo wakijitenga na mikutano ya naibu huyo licha ya kwamba uwepo wao unahitajika.

## Talaka inavyochangia mstari wa maisha na ndoa kupasuka Z'bar

**INATOKA UK. 12**

"Kama utafanya tathmini, waathirika zaidi ni wale watoto wanaolelewa na mzazi mmoja baada ya ndoa kuvunjika," anasema.

### UKUBWA WA TATIZO

Mahakama ya Kadhi Mkoa wa Kaskazini Unguja, ambayo ni mahsusi kushughulikia masuala ya dini ya Kiislamu kama ndoa, mirathi matunzo ya watoto na talaka, ina takwimu ya kuwapo kesi za madai ya talaka 421 zilizofunguliwa katika mkoa huo katika kipindi cha miaka miwili iliyopita, yaani 2020 na 2021.

Hata hivyo, idadi hiyo ya kesi ni zilizofikishwa mahakamani, huku kukiwapo talaka zinazotolewa bila kufikishwa mahakamani.

Kati ya kesi zilizofunguliwa katika kipindi hicho, mahakama ilivunja ndoa 371 kutokana na sababu mbalimbali sawa na asilimia 88.1 ya madai yote ya talaka yaliyofunguliwa katika mkoa huo.

Mufti Mkuu wa Zanzibar, Sheikh Saleh Khaabih, anasema baada ya kuona kun aongezeko la talaka, wameamua kuanzisha chuo cha mafunzo ya ndoa ili kukabiliana na changamoto ya wimbi la talaka.

Sheikh Khaabih, anaitaka jamii izingatie na kuzifuata taratibu za ndoa, kupunguza migogoro ya ndoa ikiwemo watoto kutelekezwa na kukosa huduma muhimu ikiwemo haki ya kupata elimu na matunzo.

Mhubiri wa masuala ya dini ya Kiislamu, Amina Khalfan, anasema, baada ya ndoa kuvunjika kunapaswa kuwepo usimamizi mzuri wa kuwalea watoto na kuhakikisha wanapata huduma zinazostahiki hasa haki ya elimu.

Mwanasheria kutoka Jumuiya ya Wanasheria Wanawake Zanzibar (ZAFELA), Time Asaa Khamis, anawashauri wanandoa kukimbilia katika vyombo vya sheria kunapotokea migogoro baina yao ili kupata ushauri kabla ndoa kuvunjika.

Kadhi wa Mahakama ya Wilaya Kaskazini 'B', Omar Ali, anawashauri wanandoa wanapokuwa na migogoro kuacha kukimbilia kuachana badala yake wafike mahakama ya kadhi kupata msaada wa kisheria.

Mkurugenzi Idara ya Elimu na Mafunzo ya Watu Wazima, Mashavu Ahmada, anasema baada ya kugundua watoto wengi wapo nje ya mfumo wa elimu, serikali imeanza kuchukua hatua za kuwarejesha shuleni.

"Tuliwatumia masheha kuwagundua walipo watoto hawa na kuwakusanya pamoja, baadaye tuliwachukua na kuwarejesha shule. Kwa sababu tatizo kubwa ni wazazi wao kutokuwa na uwezo wa kuwahudumia, tunawapatia vifaa vyote vya shule," anasema.

Wizara hiyo kwa kushirikiana na Shirika la Elimu kwa Wote la Qatar (EAC) inatarajia kuwarejesha shuleni zaidi ya wanafunzi 35,000 wa Unguja na Pemba katika kipindi cha miaka minne ijayo.

JUKWAA LA VIONGOZI

MADELEINE ALBRIGHT

# Mwanamke wa shoka anayekumbukwa kwa misimamo yake ya kidiplomasia

**Na Christina Mwakangale**

• Asili yake Czechoslovakia, akang'ara USA

DUNIA imempoteza mwanasiasa, mwanaharakati, mwanamke wa shoka, Madeleine Albright, ambaye aliweka historia ya kuwa Waziri wa kwanza wa Mambo ya Nje wa Marekani.

Madeleine (84), amefariki dunia wiki iliyopita na kuthibitishwa na binti yake Anna, akisema mama yake amefariki dunia baada ya kuugua saratani.

Asili ya Madeleine ni mhamiaji kutoka Czech, aliingia Marekani na kufanikiwa kuteka ulingo wa kisiasa kwa umahiri wake wa kuchambua vyema masuala ya dunia na baadae kuwa mtetezi mkuu wa sera za Rais Bill Clinton.

Historia ya Marekani haiwezi kukosa kumtambua mwanamama huyu, mtoto wa wakimbizi Waki Czech aliyekimbia kutoka kwa wavamizi wa Nazi na wakandamizaji wa Kikomunisti.

Mama huyo alifanikiwa sana kidiplomasia na kushika nyadhifa mbalimbali za kimataifa ikiwamo uwakilishi wa nchi yake Umoja wa Mataifa (UN), kuanzia mwaka 1993 hadi 1997, pia Katibu Mkuu Ikulu, mwaka 1997 hadi 2001.

Kwa nafasi hiyo (Waziri wa Mambo ya Nje) alivunja rekodi ya taifa kubwa kiuchumi duniani kwa kuwa mwanamke mwenye wadhifa huo.

Wanadiplomasia na viongozi mbalimbali duniani kote wanaendelea kutuma risala za rambirambi kwa familia ya Madeleine, zikiongozwa na viongozi waastafu wa Marekani, akiwamo Bill Clinton, George Bush, Barack Obama na Rais wa sasa Joe Biden.

Salamu za rambirambi zilizoko zinabainisha alichokiacha Madeleine ni kumbukumbu na alama ya utumishi wake bora kwa umma.

Rais Obama, anasema Madeleine alifungua njia za maendeleo katika maeneo mbalimbali ya dunia, kama vile migogoro na alikuwa bingwa wa maadili ya kidemokrasia.

Makao Makuu ya Umoja wa Mataifa, ambako Madeleine, alihudumu katika nafasi ya balozi kuanzia mwaka 1993 hadi 1997, kulikuwapo na utulivu kwa dakika moja, ikiwa ni ishara ya kumpa heshima yake mama huyo wa diplomasia.

"Ni viongozi wachache wamekuwa mahiri wakati wa kuhudumu kwao, kwa sababu alijua moja kwa moja kwamba maamuzi ya sera Marekani yalikuwa na uwezo wa kuleta mabadiliko katika maisha ya watu ,duniani kote, aliona kazi zake kama jukumu na fursa," anaeleza Rais Clinton.

Katibu Mkuu wa sasa wa Jumuiya ya Kujihami ya Magharibi (NATO), Jens Stoltenberg, anamuelezea ni mjenzi wa jeshi la uhuru na bingwa wa NATO, huku Rais wa zamani wa Marekani, George W. Bush anasema kuwa mama huyo aliweka mbele umuhimu wa jamii huru, kwa ajili ya amani duniani.



Waziri wa kwanza wa Mambo ya Nje wa Marekani, mwanasiasa, mwanaharakati, mwanamke wa shoka, Madeleine Albright. **PICHA: MTANDAO**

> Ukraine ina haki ya uhuru wake, bila kujali majirani zake ni nani. Katika enzi ya kisasa, nchi kubwa zinakubali jambo hilo.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Uingereza, Liz Truss aliandika katika ukurasa wake wa tweeter kwamba "Dunia inahitaji kuwa na maadili ya Madeleine hata zaidi ya hapo awali,"

### ASILI ALIKOTOKA

Madeleine, anaelezwa kuwa ni mzaliwa wa mji wa Marie Jana Korbelova huko Prague mwaka 1937, wakati huo ilikuwa taifa la Czechoslovakia.

Alikuwa binti wa mwanadiplomasia wa Czechoslovakia, ambaye alilazimishwa kwenda uhamishoni baada ya nchi yake kuvamiwa na Manazi wa Ujerumani mwaka 1939.

Mama huyo alihamia Marekani mwaka 1948, familia yake ilikoomba hifadhi ya kisiasa, ikisema kwamba haikuweza kurudi nyumbani kama wapinzani wa utawala wa Kikomunisti wa nchi yao wangedumu.

Madeleine, alipata uraia wa Marekani mwaka 1957 na amefanya kazi Ikulu ya White House, wakati wa utawala wa Rais Jimmy Carter na baadaye akawa Mshauri wa Sera za Kigeni kwa wagombea kadhaa wa Makamu wa Rais na Rais.

### ALIKONYANYUKIA

Mara tu baada ya Bill Clinton kutangazwa kuwa Rais mwaka 1993, Madeleine aliteuliwa kuwa Balozi katika Umoja wa Mataifa na huo ndio wadhifa wake wa kwanza wa kidiplomasia.

Kama mwanadiplomasia, Madeleine, akasaidia kurejesha amani baada ya Jamhuri ya Usovieti wakati wa utawala wa Rais Clinton, akitumia kile alichokiita 'Pragmatic Idealism' ili kuvuka maji ya kijiografia ambayo hayajajulikana.

Wakati fulani sera za kigeni akiwa kwenye wadhifa huo wa mambo ya nje, zilitumika nguvu za kijeshi za Marekani katika maeneo kama vile Irak na Balkan, wakati diplomasia iliposhindwa kufanya kazi.

Kampeni za mabomu ya NATO katika majimbo ya zamani ya Yugoslavia, yalisaidia kufanua jukumu lake baada ya Soviet kufa.

Madeleine, pia alikuwa bingwa wa kuikuza jumuiya ya NATO, akisimamia kuongezwa kwa Poland, Hungary na Jamhuri ya Czech mwaka 1999, ambayo athari zake zinaonekana hadi leo.

Mwaka 1997, alikuwa Waziri wa Mambo ya Nje, akiwashinda upinzani kutoka kwa kile ambacho wengine walikiita baadaye kuwa kikundi kisichokuwa na chochote isipokuwa Madeleine.

Alipata umaarufu zaidi wakati wa juhudi zake za kushinikiza utawala wa Rais Clinton kuingilia kati kukomesha mauaji huko Kosovo yaliyofanywa na serikali ya Serbia ya Slobodan Milosevic.

Wakosoaji wengine waliita kampeni hiyo kuwa 'Vita vya Albright' Madeleine wakati wa uhai wake akifafanua: "Nachukua jukumu hasa kwa kuamini ilikuwa muhimu kwetu kutosimama na kutazama kile Milosevic alikuwa akipanga kufanya," Akaongeza: "Hatuwezi kutazama uhalifu dhidi ya ubinadamu".

Hatimaye, Kosovo ilitangaza uhuru wake kutoka kwa Serbia mwaka wa 2008, miaka tisa baada ya kuingilia kati kwa washirika."

Rais wa nchi hiyo amesema kwamba wamepoteza rafiki wa thamani na mwenye mchango wa kweli katika uhuru na demokrasia nchini mwake na kusisitiza hautasahaulika kamwe.

Mwaka 2012, Rais wa wakati huo, Barack Obama alimtunukia Nishani ya Urais ya Uhuru, tuzo ya juu zaidi inayopatikana kwa raia kutokana na kazi yake huko Balkan.

Mwezi mmoja tu uliopita, katika usiku wa kuamkia uvamizi wa Ukraine, nyota ya Madeleine ilirejea tena hadharani huku tahariri ya New York Times ikimlenga Rais wa Russia, Vladimir Putin, ambaye alikutana naye kwa mara ya kwanza mara tu alipoingia madarakani mwaka 2000.

"Ukraine ina haki ya uhuru wake, bila kujali majirani zake ni nani. Katika enzi ya kisasa, nchi kubwa zinakubali jambo hilo," aliandika na kuongeza: Huu ni ujumbe unaosisitiza diplomasia ya hivi karibuni ya Magharibi.

"Inafafanua utofauti kati ya ulimwengu unaotawaliwa na utawala wa sheria na ambao hauwajibiki kwa kanuni zozote." ilisema taarifa hiyo.

*•Ni kwa mujibu wa mtandao.*

# Sheria yaja kudhibiti ukatili mitandaoni

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imesema inakusudia kutunga sheria ya kudhibiti ukatili wa mitandaoni kutokana na kushamiri kwa vitendo hivyo nchini.

Aidha, imeanza kufuatilia taasisi inayojihusisha na utoaji mimba ili kuichukulia hatua kwa kuwa inakiuka haki za mtoto kuishi tumboni mwa mama yake.

Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza kuhusu mafanikio 17 yaliyopatikana kwa wizara hiyo ndani ya mwaka mmoja wa uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan.

Dk. Gwajima alisema Kamati ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii wameliona suala hilo la ukatili wa mitandaoni na kulijadili ili kutungwa sheria. "Itatungwa sheria kabisa itakayodhibiti hivi vitendo, lakini niseme tu iwe aibu kwa wale watumiaji wa mitandao, unajua unavyomkatili mtu na wewe unakuwa sehemu ya watu ambao afya ya akili yako haijakaa vizuri."

"Unaweza kuwasilisha taarifa yako tu unavyotaka iwe kuliko kumkatili mtu, ukatili mwingi tu mimi nakatiliwa, huyu anakatiliwa kila mtu anakatiliwa, tunapokwenda kuitengeneza sheria tujipe moyo kuongoza watu ni kazi ngumu, Mitume waliongoza walikatiliwa kweli kweli ingawa mitandao haikuwepo, hata Mungu anakatiliwa watu wanaamka wanasema maneno wanayojua wao," alisema.

"Tujipe moyo uongozi upo, lakini sheria tunakwenda kuitekeleza na sisi tupo ngangari tunakwenda kama uongozi upo moyoni hata ukatili hutauona, aliyeamua kukukatili anatekeleza lake na kusudi lake alilotumwa na moyo wake na wewe unatekeleza lako na Mungu wako vaa miwani ya mbao, watendee wale wanyonge ambao wanakutegemea kwa wakati wa sasa."

Kuhusu vitendo vya ukatili kwa wanawake na watoto nchini, Dk. Gwajima alisema kutokana na familia kuficha taarifa za ukatili unaofanywa na ndugu wa familia, serikali inakuja na mkakati mpya wa kuwa na mfumo wa uangalizi kwenye jamii ili kukomesha tabia ya masuala hayo kumalizwa mtaani badala ya kufikishwa kwenye vyombo vya sheria.

Akizungumzia mafanikio, Waziri Gwajima alisema katika kipindi cha Machi 2021 hadi Februari 2022, kamati za ulinzi wa wanawake na watoto 1,843 zimeanzishwa na kufikia 18,186 kati ya 20,750 zilizokusudiwa kuanzishwa kuanzia ngazi ya kijiji/mtaa hadi taifa ifikapo Juni 2022.

"Serikali imeweka walimu wa unasihi katika shule za msingi na sekondari ambao wanatumika kama moja ya njia ya kutoa elimu kwa watoto kuhusu vitendo vya ukatili na kuwasaidia kuibua vitendo vya ukatili ambavyo wanafanyia shuleni au nyumbani ili kuwasaidia," alisema.

## Watakiwa kuwasilisha michango ya watumishi mifuko ya hifadhi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

NAIBU Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Atupele Mwakibete, amewataka viongozi wa wizara hiyo kuwasilisha kwa wakati michango ya watumishi kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii ili kuwaondolea adha wanapostaafu.

Mwakibete, alibainisha hayo juzi alipokuwa akifungua kikao cha Baraza la Wafanyakazi wa wizara hiyo sekta ya uchukuzi kinachofanyika jijini hapa.

Alisema, kitendo cha michango ya watumishi wa umma kutowasilishwa kwenye mifuko kumekuwa kunasababisha malalamiko mengi kwa wastaafu kukosa mafao kwa wakati.

"Unakuta mtumishi wa umma kafanya kazi serikalini kwa umri wake wa miaka 50 au 60, lakini akistaafu mafao inakuwa shida," alisisitiza Mwakibete.

Pia, aliagiza mikataba yote ya ununuzi wa umma inayofanywa na wizara hiyo izingatie sheria.

Kwa upande wake, Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Gabriel Migire, alisema lengo la kikao hicho ni kujadili utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha 2021/2022 pamoja na bajeti ya 2022/2023.

Alisema katika bajeti ya mwaka 2022/2023 sekta ya uchukuzi imetengewa Sh. trilioni 2.4 kwa ajili ya matumizi mbalimbali ya maendeleo ikiwamo kuendelea na ujenzi wa reli ya kisasa (SGR).

Pia, alisema kazi nyingine ni kufanya ukarabati na kuweka miundombinu ya usalama kwenye maziwa na kiasi cha Shilingi bilioni nne kutoka Benki ya Dunia kitatumika.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Selemani Jafo (katikati), akizungumza wakati wa upandaji miti katika kampeni ya wasaa wa mazingira, wilayani Kisarawe, mkoani Pwani mwishoni mwa wiki, yenye lengo la kuhamasisha upandaji miti ili kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi, ambapo wadau wa mazingira Taasisi za Vodacom Tanzania Foundation na WWF wameshirikiana kupanda na kusimamia miti wilayani humo. Kushoto ni Meneja wa Vodacom Tanzania Foundation, Sandra Oswald. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Chamwino yaombwa kupunguza kero shule za msingi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

HALMASHAURI ya Chamwino Mkoa wa Dodoma imeombwa kuiangalia sekta ya elimu katika bajeti ijayo 2022/23 ili kupunguza kero 10 zinazowakabili wanafunzi hususani wa shule za msingi.

Kero hizo ni pamoja na upungufu wa matundu ya vyoo hali inayosababisha baadhi ya shule wanafunzi kujisaidia kwa foleni na kushindwa kuhudhuria vipindi vya darasani ipasavyo.

Mwenyekiti wa klabu za wanafunzi ambaye pia ni mwanafunzi wa Shule ya Sekondari Mlowa, Wema Nollo, aliyasema hayo jana alipokuwa akiwasilisha mapendekezo kwa uongozi wa halmashauri hiyo kwenye mkutano wa wadau wa elimu ulioandaliwa na Shirika lisilo la kiserikali la Action Aid Tanzania kupitia mradi wake wa boresha elimu kwa Mikoa ya Singida na Dodoma.

Alisema kuna shule ina wanafunzi zaidi ya 1,000, lakini matundu ya vyoo yaliyopo ni sita.

"Unakuta shule moja ina wanafunzi zaidi ya 1,000 na ina matundu sita wasichana matatu na wavulana matatu, muda wa mapumziko ni dakika 20 wanaoenda kujisaidia ni wengi na msongamano ni mkubwa na muda wa vipindi unakuwa tayari umefika hii husababisha kuchelewa vipindi na wakati mwingine inasababisha kupata magonjwa kama UTI," alisema.

Alitaja kero nyingine ni ukosefu wa vyumba vya faragha, uhaba wa maji, nyumba za walimu, upungufu wa walimu wa masomo ya sayansi katika shule za Sekondari na miundombinu mibovu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum.

Akizungumzia kero ya umbali, mwanafunzi wa Shule ya Msingi Buigiri, Editha Mabwe, aliomba serikali kuwajengea mabweni au shule karibu na vijiji ili kupunguza utoro na kukuza taaluma katika halmashauri hiyo.

"Shule nyingi za Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino zimejengwa mbali na wakazi wa kijiji kwa mfano Chilonwa, kuna wanafunzi wanatoka Mlimwa wanakuja kusoma Shule ya Sekondari Chilonwa, kuna wanafunzi wanatoka Kijiji cha Chiwahele wanakuja kusoma Buigiri, hali ile inawasababishia wanafunzi kupata changamoto mbalimbali ikiwamo wasichana kurubuniwa na kupata mimba za ututoni," alisema Mabwe.

Hata hivyo, Mwenyekiti wa halmashauri hiyo, Edson Sweti, alisema mapendekezo hayo watayafanyia kazi ili kuwaondolea kero wanafunzi.

"Tutashauriana na wenzetu hawa ili asilimia kubwa ya bajeti iende kwenye matundu ya vyoo, tunapotoka hapa tunaenda kuyafanyia kazi kwa kuwa changamoto hizi zimeanzia nyuma huko," alisema.

Ofisa Elimu Sekondari wa wilaya hiyo, Tulinagwe Ngonile, alikiri kuwapo kwa kero hizo na na kuahidi kuwa kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wamejipanga kuzitatua.

"Hivi sasa hivi tuna miradi mbalimbali katika ngazi ya sekondari tuna mradi wa kuboresha elimu ya sekondari, kupitia mradi huu tutaenda kufanya ujenzi wa miundombinu, tutajenga shule mpya, lakini pia tutaongeza miundombinu kama vile maabara, vyoo na madarasa, kwa hiyo hii changamoto ya vyoo sasa itakuwa historia," alisema Ngonile.

"Mfano kwenye bajeti yetu ya mwaka wa fedha ujayo tuna jumla ya madarasa 53 ambayo tumetengewa kwa ajili ya shule zetu za Msingi hiyo itasaidia kupunguza msongamano wa wanafunzi madarasani, pia kuna mradi ambao unajenga matundu ya vyoo 150 kwa shule zetu za msingi tumeelekeza kupeleka katika shule zenye changamoto," alisema.





# Mvua yaezua nyumba, yaharibu mazao

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MVUA iliyokuwa imeambatana na upepo pamoja na mawe imeezua nyumba za wananchi na kuharibu mazao katika kijiji cha Holongo, Kata ya Igale Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya.

Tukio hilo lilisababisha baadhi ya wananchi kunusurika kuangukiwa na kuta za nyumba. Mvua hiyo ilinyesha juzi jioni ambapo kwa mujibu wa wananchi hao, ilinyesha kwa muda usiozidi saa moja na nusu, lakini ikaleta madhara makubwa na kwamba hata miundombinu ya barabara imeathiriwa.

Mmoja wa wananchi hao, Rebeca Wilson, alisema wakati mvua hiyo inaanza kunyesha alikuwa amekaa ndani na watoto wake wawili pamoja na wajukuu watatu.

Alisema baada ya nyumba kuezuliwa na ukuta mmoja kuanguka, ndipo alianza kukimbia na watoto wake kwenda kujisitiri jikoni na kwamba mpaka sasa wanaishi humo liche ya kuwa na familia kubwa.

Rebeca alisema baada ya nyumba hiyo kuezuliwa vitu vyake vyote viliharibika, hivyo mpaka sasa hana chochote huku mazao aliyokuwa amepanda shambani yakiwa yameharibika.

"Naomba wasamaria wema wanisaidie kuezeka nyumba yangu maana mabati yote yameharibika na hata chakula sina, nahangaika sana, hata jiko ambalo nimehamia linavuja sana," alisema Rebeka.

Naye Enea Mwabhela alisema wakati nyumba yake inaezuliwa alikuwa amekaa ndani na watoto wake, huku mume wake ambaye ni mlemavu akiwa amelala chumbani.

Alisema mabati ya nyumba hiyo yaliezuliwa na kupelekwa umbali wa zaidi ya mita tano kutoka ilipo nyumba hiyo hali ambayo ilisababisha zikaharibika na hazifai kutumika tena.

Alisema baada ya nyumba kuezuliwa amehamia kwenye pagala pamoja na familia yake ambapo alisema nyumba hiyo ni ndogo na haifai kuishi na familia kubwa.

"Chakula chote kimeharibika na nimekuwa na mzigo mkubwa maana majukumu yote ya familia yananikabili mwenyewe, mume wangu hana kazi yoyote kwa sababu ni mlemavu wa mkono mmoja ambao ulikatwa," alisema Enea.

Alisema liche ya nyumba yake moja kuezuliwa lakini jiko ambalo walihamia nalo limebomoka ukuta mmoja hali ambayo inaifanya iwe hatari kwa maisha yake na familia nzima.

Mwenyekiti wa Kijiji hicho cha Holongo, Meshack Mayasu, alisema kijiji hicho kina vitongoji vinane lakini vilivyoathirika na mvua huo ni vitongoji sita na viwili pekee ndivyo vilivyopona.

Alisema mazao yaliyoathirika na mvua hiyo ni mahindi, kahawa na maharage ambayo alisema yalikuwa bado hayajakomaa na hivyo kuna hatari wananchi hao wakakumbwa na njaa pamoja na kuporomoka kiuchumi.

Alisema ili kukabiliana na ukali wa maisha wanawaomba wadau mbalimbali ikiwamo serikali kuwasaidia wananchi hasa ambao nyumba zao zimeezuliwa wasaidiwe.

"Tunamwomba hata mbunge wetu wa Jimbo la Mbeya Vijijini, Oran Njeza, atusaidie kuwafariji wananchi hawa maana hali sio nzuri, mazao yameharibika sana, kahawa yote ipo chini na maharage yameharibika kabisa," alisema Mayasu.



Ofisa TEHAMA wa Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA), Thomas Hoya (kushoto), akieleza namna mfumo mpya wa malipo ya ushuru wa maegesho, utakavyoanza kufanya kazi Aprili mosi mkoani Mbeya, katika studio za redio Ushindi Fm, zilizoko mkoani humo jana. Wengine ni maofisa wa wakala huo. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Watakiwa kulipia maegesho kidigitali

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WATUMIAJI wa vyombo vya moto mkoani Mbeya, wametakiwa kuzingatia utaratibu mpya wa malipo ya ushuru wa maegesho kidigitali ili kuchangia maendeleo ya maboresho ya barabara.

Kauli hiyo ilitolewa jana na mhasibu wa kitengo cha mapato kutoka Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TATURA) Mkoa wa Mbeya, Abel Ilomo, wakati akitoa elimu juu ya mfumo mpya wa ulipaji ushuru wa maegesho kidigitali katika kituo cha redio cha Ushindi FM.

Ilomo alisema kila mtumiaji wa chombo cha moto mkoani Mbeya, anapaswa kulipa ushuru wake kwa kidigitali kupitia mitandao ya simu na benki.

Alisema kwa yeyote atakayekaidi atachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria za TARURA ambazo zinawataka watumiaji wa vyombo vya moto mkoani humo kulipa ushuru kwa mujibu wa sheria.

"Mbeya ni miongoni mwa mikoa inayoanza utekelezaji wa mfumo mpya wa malipo ya ushuru wa maegesho kidigitali Aprili mosi mwaka huu, matarajio yetu ni watumiaji wa vyombo hivyo kulipa ushuru kwa wakati ili kuepukana na mkono wa sheria pamoja na faini ya Sh. 10,000 baada ya siku 14 kupita bila kulipa fedha," alisema.

Ofisa Uhusiano kutoka TARURA, Anitha Wande, alisema mfumo huo wa kidigitali una manufaa makubwa kwa watumiaji wa vyombo vya moto kwani inarahisisha malipo na kuziba mianya ya rushwa.

Alisema kuanzishwa kwa mfumo huo kusaidia kuongeza mapato ya nchi na kusababisha ujenzi wa miundombinu ya barabara maeneo mbalimbali nchini.

Aliwataka watumiaji wa vyombo vya moto kuwa waaminifu kulipa malipo ya maegesho kwenye maeneo rasmi yaliyotengwa katika kila eneo la mji.

Naye Hussein Nzally, Mhasibu wa Kitengo cha Maegesho, TARURA makao makuu Dodoma alisema mfumo huo mpya wa malipo wa maegesho ya vyombo vya moto ni rafiki kwa kuzingatia hali za Watanzania.

Alisema pikikipi ya magurudumu mawili (bodaboda), ushuru wake wa maegesho kwa saa ni Sh. 300 kutoka 200 iliyokuwa awali kabla ya mfumo mpya kwa wiki Sh. 1,500 na kwa mwezi Sh. 6,000.

Bajaji kwa siku ushuru Sh. 500 kwa wiki Sh. 2,500 na kwa mwezi 10,000 huku gari ikiwa Sh. 300, kwa siku 1,000, wiki Sh. 5000 na mwezi Sh. 20,000.

Kwa upande wake, Ofisa TEHAMA wa TARURA, Thomas Hoya, alisema kwa sasa mfumo wa malipo utatumika kwa benki mbili tu ambazo ni CRDB na NMB.

## Wadau TMDA sasa wahimizwa taratibu

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

KAIMU Meneja wa Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Anitha Mshighati, amewakumbusha wadau wa mamlaka hiyo, kuzingatia utaratibu wa kuingiza na kutoa bidhaa nchini ili kulinda afya za wananchi.

Mshighati alitoa kauli hiyo jana akizungumza na Nipashe juu ya mwitikio wa wafanyabiashara wa dawa za binadamu katika kuzingatia sheria za uingizwaji wa bidhaa nchini.

Alisema miongoni mwa mambo wanayopaswa kuzingatia wafanyabiashara hao ni kuwa na nakala ya kielektroniki ya taarifa ya mzigo mfano Ankara, kifani pamoja na vibali kutoka taasisi nyingine zinazohusika na usajili.

Alisema wafanyabiashara hao wanatakiwa kuhakikisha wanajaza fomu ya usajili ya mteja na kuiwasilisha Ofisi za TMDA ili kupata namba ya utambulisho na nywila.

Aliongeza kuwa kabla ya muhitaji kulipa ada ahakikishe anawasilisha hati ya malipo ambayo yatafanyika benki katika ofisi ya TMDA ili kupata kibali za kufanya biashara hiyo ya uingizwaji wa bidhaa anazozihitaji.

"Tunahamasisha wafanyabiashara wanaojihusisha na uuzaji wa dawa za binadamu kuzingatia utaratibu na sheria za kuingiza na kutoa bidhaa nchini ili kulinda afya za watumiaji," alisema Mshighati.

Aliwahamasisha wafanyabiashara kuzingatia usajili wa dawa nchini kujihakikishia kuwa zinakidhi viwango vya ubora, usalama na ufanisi ili watumiaji waweze kupata dawa sahihi kwa ugonjwa husika.

Alisema dawa husajiliwa kwa lengo la kuwalinda watumiaji wasidhurike kutokana na madhara yanayoweza kujitokeza kwa kutumia dawa zisizokidhi viwango vya ubora na usalama.

Alifafanua kuwa dawa zote zinazosajiliwa hudumu kwa miaka mitano endapo kama haitabatilishwa au kuahirishwa na baada ya kipindi hicho mfanyabiashara anaweza kuomba kuendelea na usajili wa dawa hiyo kwa kufuata taratibu kama zilivyoelekeza katika mwongozo wa usajili wa dawa.



# Nyaraka, makumbusho yatakiwa kujitegemea

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais Ikulu, Jamali Kassim Ali, ameutaka uongozi wa nyaraka na makumbusho kujitegemea katika uendeshaji wa taasisi hizo ili kuongeza pato la taifa.

Kassim alitoa maelekezo hayo alipotembelea jengo la makao makuu ya taasisi hiyo Kikwajuni Mjini Zanzibar na kuzungumza na uongozi na watendaji wa ofisi hiyo.

Alisema wakati umefika kwa taasisi hiyo kujenga mazingira mazuri ambayo yataifanya kujitegemea na kuwa ya moja ya vitega uchumi vya Zanzibar katika sekta ya nyaraka.

Alisema zipo baadhi ya nchi duniani zimeingiza mapato makubwa kutokana na sekta ya nyaraka ambayo husaidia watu mbalimbali ikiwamo wasomi kufanya utafiti.

Alisema Zanzibar imejaliwa kuwa na nyaraka muhimu za ukumbusho wa mambo ya kale ambazo hutumiwa na watu mbalimbali, wakiwamo watafiti kufanya kazi zao za kitaalamu.

Aidha, alisema Zanzibar imejaliwa kuwa na makumbusho ya kale ambayo yamebeba historia kubwa, ikiwamo ya utumwa kwa tawala mbalimbali zilizopata kuongoza Zanzibar.

"Ndiyo maana nasema wakati umefika sasa kugeuza makumbusho ya kale na nyaraka zetu kuwa kivutio kwa wageni kuja nchini na kufanya utafiti wa kisomi," alisema.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa Nyaraka na Kumbukumbu, Khatib Suleiman Khatib, alisema wamejipanga vizuri kuhakikisha nyaraka zinatunzwa na hakuna njia ya kutumiwa kinyume cha sheria ikiwamo upotevu.

Hata hivyo, alitaka juhudi zaidi zichukuliwe katika njia bora za utunzaji wa nyaraka ikiwamo vifaa vya kisasa vitakavyotumika kuhakikisha nyaraka zinadumu kwa muda mrefu.




Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Bluu Amber, Grant Anderson (kushoto), akibadilishana hati na Mkurugenzi wa Taasisi ya Sauti za Busara, Yussuf Mahmoud, jijini Zanzibar jana, baada ya kusaini makubaliano ya kufadhili Tamasha la Sauti za Busara. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## ACT yataka wanawake kugombea uongozi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WANAWAKE wa Chama cha Act-Wazalendo wametakiwa kujitokeza kuwania nafasi za uongozi katika chama hicho ili kuhakikisha usawa wa kijinsia unafikiwa kwa makundi yote.

Makamu Mwenyekiti wa chama hicho, Othman Masoud Othman, alitoa kauli hiyo alipozungumza na ngome ya wanawake wa chama hicho kwa nyakati tofauti maeneo ya Donge na Mjini Magharini Unguja.

Alisema wanawake bado wapo nyuma katika kujitokeza kuwania nafasi za uongozi licha ya kwamba ushiriki wao katika harakati za chama na kisiasa ni mkubwa.

Alisema katika mwaka 2020 ni wanawake wanane pekee waliojitokeza kuwania nafasi za uongozi katika ngazi za kuchaguliwa za uwakilishi na ubunge.

Alisema katika kuelekea Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025 wamejipanga kuhakikisha idadi ya wanawake wanaowania nafasi za uongozi inaongezeka, huku akisisitiza kwamba hakuna vikwazo dhidi yao ya kushiriki nafasi hizo.

"Ushiriki wa wanawake katika kuwania nafasi za uongozi kwa upande wa chama chetu hauridhishi...katika uchaguzi wa mwaka 2030 ni wanawake 8 tu waliowania nafasi za uongozi za kuchaguliwa katika majimbo ya uchaguzi," alisema.

Othman ambaye ni Makamu kwa Kwanza wa Rais wa Zanzibar aliwapongeza wanawake kwa kuonyesha utayari wa kushiriki katika harakati za kisiasa na kuimarisha ngome ya wanawake kisiasa zaidi.

Alisema ACT-Wazalendo inaunga mkono juhudi za wanawake katika ushiriki wa siasa nchini, hivyo kuwaunga mkono kwa nguvu zote.

Naye Naibu Katibu wa Haki za Binaadamu katika chama hicho, Pavu Abdalla Juma, aliwataka wanawake kamwe wasikate tamaa na kujitokeza kujiunga katika ngome za wanawake katika siasa kwenye majimbo yote ya Unguja na Pemba.

Aidha, aliwataka wanawake kuunga mkono maridhiano ya kisiasa ambayo kwa kiasi kikubwa yamesaidia kundi la wanawake kufanya harakati za kisiasa bila ya vikwazo, tofauti na mwaka 2020.

# SMZ kuendelea kuyapa kipaumbele matamasha

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imeahidi itaendelea kuunga mkono matamasha kuhakikisha yanaendelea kubakia, kwa sababu yana mchango mkubwa katika kukuza uchumi na kuendeleza sekta ya utalii.

Ahadi hiyo ilitolewa jana na Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Khamis Abdallah Said, wakati akizungumza katika hafla ya kutia saini udhamini kati ya kampuni ya Blue Amber Zanzibar na Shirika la Sauti za Busara.

"Tulishtuka sana baada ya kusikia tamasha la Sauti za Busara linasitisha shughuli zake kuanzia Machi 31, mwaka huu, kutokana na wafadhili Ubalozi wa Norway kumaliza muda wao, lakini leo tunafarijika kuona wafadhili wengine wamejitokeza kuendeleza tamasha hilo," alisema.

Hata hivyo, alisema kwamba wakati umefika kwa Tamasha la Sauti za Busara kuandaa mpango kazi kwa kushirikiana na serikali ili kujitegemea badala ya kutegemea wafadhili.

Alisema kwamba Tamasha la Sauti za Busara lina mchango mkubwa katika maendeleo ya sekta ya utalii, kuendeleza utamaduni, kutoa ajira kwa vijana pamoja na kutangaza utamaduni wa Zanzibar.

"Zipo fursa nyingi za kuweza kujenga uwezo wa kujitegemea kwa kushirikiana na wadau wanaonufaika na matamasha yanayofanyika Zanzibar hasa wakati huu serikali ikiwa imo katika utekelezaji wa mpango wa uchumi wa bluu," alisema.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Bluu Amber, Grant Anderson, alisema kwamba kampuni hiyo imeamua kudhamini tamasha hilo kwa muda wa miaka mitatu baada ya kuguswa na taarifa za tamasha hilo kuwa katika hatari ya kufa kutokana na kukosekana kwa wafadhili.

"Tulipopata taarifa kuwa Tamasha la Sauti za Busara linafunga milango yake kutokana na kukosa udhamini, tulichochewa kuchukua jukumu la kuokoa tamasha hilo na sasa tunatangaza rasmi uzamini wa muda wa miaka mitatu," alisema.

Alisema kwamba tamasha hilo kubwa Afrika ambapo mwakani wataadhimisha kufikisha miaka 20 na limefanya kazi kubwa kwa kuunganisha muziki wa Afrika na kuleta umaarufu kwa Zanzibar na kusaidia mamia ya wafanyabiashara na kuendeleza utalii.

Kwa upande wake waanzilishi wa kampuni hiyo, Sleh Muhammed Said, alisema wameamua kufadhili tamasha hilo baada ya kusikia taarifa kuwa lipo katika hatari ya kusitisha shughuli zake mwaka huu.

"Tamasha la Sauti za Busara ni kielelezo kikubwa cha kuendeleza utamaduni na limekuwa likitoa mchango mkubwa katika kukuza uchumi wa Zanzibar na kuleta maendeleo katika sekta ya utalii," alisema.

Mkurugenzi wa Sauti za Busara, Yussuf Mahmoud, alisema baada ya kupatikana wafadhili sasa tamasha hilo litaendelea kama kawaida na kuishukuru kampuni ya Bluu Amber kwa kujitokeza kufadhili.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KADI YA GARI

SWEET TEST (T) LTD ANATANGAZA kupotelewa na kadi ya GARI (TATA-TRUCK) yenye namba za usajili T721 DHU. Chassis namba: MAT386534G8RI. Injini namba: 497TC93FTY824. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi RB namba IRI/IRI/RB/125665/2022.

## KUPOTEA KADI YA GARI

SWEET TEST (T) LTD ANATANGAZA kupotelewa na kadi ya GARI (TATA-TRUCK) yenye namba za usajili T514 DMA. Chassis namba: FE636E500416. Injini namba: FE536E9416. Kadi Namba: 7667744. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi RB namba IRI/IRI/RB/125669/2022.

## KUPOTEA KADI YA GARI

ELIAH ELLY JOHN ANATANGAZA kupotelewa na kadi ya GARI (TATA-TRUCK) yenye namba za usajili T554 DBR. Chassis namba: MAT357187D8R27466. Injini namba: 497SPTC35JWY647233. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi RB namba IRI/IRI/RB/125662/2022.

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**NDUGU MARIA AUGUSTINE RIMO,** Anatangaza kupotelewa na kadi yake ya Gari aina ya **SUBARU IMPREZZA** yenye no za USAJILI **T912 DVG,** kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.
TAARIFA YA POLISI: **DOD/DOD/RB/125963/2022.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA YA MBEYA**
**SHAURI LA RUFAA JINAI NA. 155/2020**
**(Asilia Shauri la Jinai Na.246/2019, Mahakama ya Hakimu Mkazi Mbeya)**

**JAMHURI........................MRUFANI**
**DHIDI YA**
**JOSEPH JUMA KYANDO............MJIBU RUFAA**

**KWA BWANA: JOSEPH JUMA KYANDO**

**POPOTE ULIPO TANZANIA.**

Unaamriwa na Mahakama hii kuhudhuria hapa Mahakamani, Tarehe 06/04/2022 siku ya JumaNne Saa3:00 Asubuhi bila kukosa.
ELEWA KWAMBA Ukikosa kufika siku hiyo Shauri litasikilizwa upande mmoja bila wewe kuwepo na Uamuzi kutolewa.
Hati hii imetolewa kwa Amri yangu na Muhuri wa Mahakama leo hii Tarehe 28 February,2022.

NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
MBEYA

**NAIBU MSAJILI**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**MBEYA**

## KUPOTEA KWA CHETI



NDUGU STEVEN MAZEMBA anatangaza kupotelewa na cheti chake cha kidato cha Nne, Index no **S.3050/0088,** Kilichotolewa na Baraza La Mitihani katika shule ya Sekondari **MPUNGUZI** Mkoa wa Dodoma Mwaka 2014, Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.
TAARIFA YA POLISI AR/RB/15159/2017.

## KUPOTEA KWA CHETI



**NDUGU FROLIAN VENANCE KADEGE,** Anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato na cheti cha chuo cha Ualimu , Kidato cha Nne Index no **S.1578-0140** Kilichotolewa na baraza la mitihani katika shule ya Sekondari Changarawe Mkoa wa Iringa Mwaka 2012.
Taarifa ya Polisi. **HAN/B1/1/19/VOL.XIII/164**
Chuo cha Ualimu No E.0603-0043 Kilichotolewa na Mufindi Teachers Collage Mkoa wa Iringa Mwaka 2015. Taarifa ya Polisi **HAN/PS/B.1/19/VOL.XIII/33**
Yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

## KUPOTEA KADI YA GARI

ISSA DAVID MWANKINA anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari yenye namba za usajili T 703 DDZ – TOYOTA COASTER. Chassis namba HZB500008930. Engine namba 1HZEAA8930. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.
Taarifa ya polisi: DAR/URA/RB/126206/2022

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**THEOPHILY MAYENGA KEBTUGUNYI** anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari aina ya **TOYOTA SPACIO** yenye namba za usajili **T772 BQW.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.
TAARIFA YA POLISI.
**DAR/CHA/RB/101465/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**CHIMWEMWE HENRY MAZUNDA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 813 BQN** – NISSAN TERRANO. Chassis namba **LR50018778.** Engine **VG338778.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.
Taarifa ya polisi:
**DOD/DOD/RB/82543/2022.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MOHAMED RAMZAN MUSSA** anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari yenye namba za usajili **T 701 DGD** aina ya **BREVIS** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi.
Taarifa ya Polisi.
**DOM/TR/RB/599/2022**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M. 1984 NYONGEZA)**
**YA KANUNI YA 2**

**Katika Mahakama ya mwanzo MIKONGENI**

**Usimamizi wa mirathi NO 03.... 2022**

**MUOMBAJI: NIA IDDI KIGONZO**
**Ombi la msimamizi wa mirathi ya marehemu IDDI HALFAN KIGONZO**

**Kwa HAKIMU MFAWIDHI**
**MAHAKAMA YA MWANZO MIKONGENI**
**S.L.P 2375**
**MVOMERO**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe: 13/04/2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo WOsia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa Tarehe 23/03/2022

Tarehe: 23/03/ 2022
SAINI YA HAKIMU

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**BAHATI SAMWEL MWAKALONGE** anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari yenye namba za usajili **T 475 BZW** aina ya **TOYOTA CRESTA.** Chassis No. **GX1006028685,** Engine **No.1G6481503.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi.
Taarifa ya Polisi.
**DOD/DOD/ RB/126240/2022.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**MAHAKAMA YA MWANZO NYANKUMBU**
**WILAYA YA GEITA**
**SHAURI LA MADAI NA: TALAKA 16/2022**

**MDAI: EDITH FRANCIS NSIIMA**
**DHIDI YA**
**MDAIWA: GERVAS KAKULU IFUNYA**
**WADAR ES SALAAM**

**AMRI:**
Unaamriwa na Mahakama uhudhurie hapa Mahakamani mnamo tarehe 5/04/2022 Saa 2:30 Asubuhi bila kukosa.
Usipohudhuria shauri hili laweza kusikilizwa upande mmoja bila ya wewe kuwepo,na kutolewa uamuzi.
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na muhuri wa Mahakama leo **JUMATANO** tarehe 23 Mwezi 2, 2022

HAKIMU
RESIDENT MAGISTRATE
GEITA

.............................................................
**HAKIMU**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA
Katika Mahakama ya Mwanzo Wilaya ya MOROGORO
Kituo cha MJINI Mkoa Wa MOROGORO
Usimamizi wa Mirathi Na...12...2022
KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA
MAREHEMU ZAKARI .E.KUWANDE WA MANZESE
KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI
YALIYOLETWA NA GODFREY ZAKARIA ELIAS

**TANGAZO**
(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 06 Mwezi 04 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Zingatia;
- Endapo kuna yoyote mwenye wosia na marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia ya narehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa.
- Marehemu hakuacha wosia
- Futa isiyohusika.

Imetolewa Tarehe 29 Mwezi 03 Mwaka 2022.


**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 0782253676**

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharasma yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA

UCHAGUZI MKUU KENYA 2022

# Ruto aonya Ikulu kutumika kuendeleza mifarakano

**Nairobi, KENYA**

NAIBU Rais wa Kenya, William Ruto amemshutumu Rais Uhuru Kenyatta, kwa kutumia Ikulu kwa shughuli za kisiasa na mazungumzo akiyataja yanakuza mifarakano.

Katika muendelezo wa vita vya maneno kisiasa, wawili hao, wameendelea kutofautiana. Ruto anasema eneo hilo, linafaa kuchukuliwa kuwa lisiloegemea upande wowote, kwa manufaa ya Wakenya wote na kuendeleza umoja wao.

"Nataka kuzungumza na ndugu yangu, Rais Uhuru Kenyatta, wewe ni kiongozi wa Wakenya wote. Usiruhusu Ikulu iwe ukumbi wa kupanda mbegu za mgawanyiko wa watu wa Kenya kwa misingi ya kijamii na kikabila," amesema Ruto, akiwa Msambweni, Kaunti ya Kwale kwenye mkutano wa kisiasa.

DP alisema ingawa Rais Kenyatta haungi mkono azma yake ya urais, hafai kutumia nafasi yake kueneza uwongo wa kisiasa na habari mbaya dhidi yake na kudai kwamba alimuunga mkono Rais Kenyatta wakati viongozi wengine wote wakiwa kinyume na Kenyatta.

Naibu Rais, anaweza kuchukua madaraka moja kwa moja kutoka kwa rais, ikiwa rais ataondolewa madarakani kwa kushtakiwa au akifa au akatangazwa kuwa hawezi kiakili kutekeleza majukumu yake.

"Nilisimama na wewe wakati hakuna mtu mwingine aliyekuwa tayari kusimama na wewe, nilikuunga mkono, wakati marafiki ulionao sasa wakiwa dhidi yako, kwamba tuliwahi kuhusishwa na mwanaume wa Kitendawili (Raila Odinga) ili kukushtaki au kuangusha serikali yako," amesema.

Amemshauri rais aiheshimu ofisi yake na kuitumia kama ishara ya umoja na si utengano.

**"Nataka kuzungumza na ndugu yangu, Rais Uhuru Kenyatta, wewe ni kiongozi wa Wakenya wote. Usiruhusu Ikulu iwe ukumbi wa kupanda mbegu za mgawanyiko wa watu wa Kenya kwa misingi ya kijamii na kikabila," amesema Ruto, akiwa Msambweni, Kaunti ya Kwale kwenye mkutano wa kisiasa.**



Rais wa Uturuki, Recep Tayyip Erdogan, akitoa hotuba ya kuwakaribisha wajumbe wa Russia na Ukraine, kabla ya kuanza mazungumzo mjini Istanbul, Uturuki, jana. **PICHA: REUTERS**

MASHAMBULIZI RUSSIA-UKRAINE:

# Dmytro Kuleba: Usile, kunywa chochote katika mazungumzo

**Istambul, UTURUKI**

MAZUNGUMZO ya kutafuta njia ya kuwakutanisha Rais wa Russia, Vladimir Putin na wa Ukraine, Volodomyr Zelensky, yameanza, mjini Istanbul, huku Rais wa Uturuki, Recep Tayyip Erdogan, akiongoza kikao hicho nchini mwake. Leo ni siku ya 35 tangu Russia ilipoanza mashambulizi Ukraine.

Wawakilishi kutoka pande mbili zinazohitilafiana kwa sera na maamuzi binafsi kama nchi huru, walifika kwenye kikao hicho, kilichoanza jana mjini humo.

Aidha, kabla ya kikao hicho, Waziri wa Mambo ya Nje wa Ukraine, Dmytro Kuleba alishauri mtu yeyote anayekwenda kwenye mazungumzo na Russia, asile au kunywa chochote, akisisitiza kuepuka kugusa sehemu yoyote.

Dmytro, ameyasema hayo wakati akizungumza kwenye mahojiano na kituo cha habari cha Ukraine, kiitwacho Ukrayina 24.

Onyo hilo lilitolewa baada ya taarifa za kushukiwa kuwekewa sumu bilionea wa Russia, Roman Abramovich na wapatanishi wa Ukraine mapema mwezi huu katika mazungumzo ya amani kwenye mpaka wa Ukraine na Belarus, ambayo hata hivyo hayakutoka na suluhu.

Hata hivyo, bilionea huyo na mmiliki wa klabu ya soka ya Chelsea ya Uingereza, ameonekana kwenye meza moja ya mazungumzo, mjini Istanbul.

Uwepo wa Abramovich kwenye kikao, unaonyesha bado anahusika katika kiwango fulani kwenye majaribio ya upatanishi.

Juzi, ripoti ziliibuka kwamba alipata dalili za tuhuma za sumu katika mazungumzo ya amani kwenye mpaka wa Ukraine na Belarus.

Mazungumzo hayo ni ya kwanza ya ana kwa ana, kufanyika mjini Istambul, tangu ya awali yaliyofanyika mpakani mwa Ukraine na Belarus, kutofikia mwafaka.

Kyiv, imesema kipaumbele chake kikubwa kwenye majadiliano ni usitishwaji wa mapigano mara moja, ingawa hadi jana mji wa Mykolaiv, umekumbwa na mashambulizi ya anga ya jeshi la Russia.

Rais Zelensky anasema vikosi vya Ukraine, vimechukua tena udhibiti wa Irpin, mji muhimu ulio karibu na mji mkuu, Kyiv.

Ukraine imesema kuwa itarejea shughuli za kuwahamisha raia kupitia njia za misaada ya kibinadamu baada ya kusimama kwa siku moja kutokana na masuala ya usalama.

### KINACHOENDELEA HADI SASA

Wakati wajumbe wakiendelea na mazungumzo hayo, Rais Zelensky ameomba mara moja mataifa yenye nguvu duniani, kuimarisha vikwazo dhidi ya Russia, ikiwa ni pamoja na vikwazo vya mafuta.

Ving'ora vya mashambulizi ya anga vilisikika kabla ya mapambazuko siku ya jana, huku maofisa wakisema, njia za kutoka katika baadhi ya miji zimezibwa na mashambulizi ya Russia.

Rais wa Marekani Joe Biden amesema hatageuza maoni yake yenye utata kuhusu Rais Putin, akisema hawezi kubaki madarakani.

Biden amesema alikuwa akielezea ghadhabu ya kimaadili anayohisi, badala ya kueleza mabadiliko ya sera.

Wizara ya Ulinzi ya Uingereza inaamini kwamba mamluki kutoka kundi la Wagner la Russia, wametumwa Mashariki mwa Ukraine na takriban wafanyakazi 1,000 wakiwa njiani.

Ofisa Mkuu wa Ulinzi wa Marekani, amethibitisha kwamba, Ukraine imefanikiwa kuuteka tena mji wa Trostyanets karibu na Sumy na kusonga mbele kwa Russia, kuelekea Kyiv kumekwama huku kukiwa na mwelekeo kuelekea eneo la Mashariki la Donbas.

Mashirika ya misaada ya Umoja wa Mataifa (UN), yamesaidia watu 900,000 nchini Ukraine hadi kufikia sasa, likieleza watoa huduma hao wahakikishiwe usalama na pande zinazozozana, msemaji wa shirika hilo la dunia amesema.

Jens Laerke, Msemaji wa Ofisi ya UN ya Kuratibu Masuala ya Kibinadamu (OCHA), amewaambia wanahabari kwamba idadi ya watu waliopewa msaada kufikia sasa ni nzuri.

**Imeandaliwa na Christina Mwakangale kwa msaada wa mtandao**

# TFF, NBC ZASAINI MKATABA BIMA YA AFYA WACHEZAJI

**Na Dennis Fussi**

BENKI ya NBC ambayo ni mdhamini Mkuu wa Ligi Kuu Tanzania Bara imezindua huduma mpya ya Bima kwa wanamichezo mahususi wachezaji, benchi la ufundi pamoja na familia zao ikilenga kuwahakikishia huduma bora za kiafya wanapatapo majanga.

Huduma hiyo inayopewa amana na Kampuni za Bima ya Britam na Sanlam inahusisha Bima ya Afya na maisha itahusisha wachezaji 640 wanaoshiriki ligi kuu, benchi la ufundi pamoja na familia zao.

Akizungumza wakati wa hafla fupi ya uzinduzi wa huduma hiyo iliyofanyika jana jijini Dar es Salaam na kuhudhuliwa na wadau mbalimbali wa mchezo wa soka hapa nchini, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NBC, Theobald Sabi, alisema pamoja na faida nyingine, bima hizo zitasaidia kuwapa wachezaji uhuru wa kuonyesha vipaji vyao bila hofu ya kupitia wakati mgumu pindi wanapopatwa na majanga uwanjani ikiwamo kuumia.

"Huduma hii itawapatia wachezaji uwezo wa kupata matibabu bora ndani na hata nje ya nchi pale itakapobidi. Zaidi pia kupitia huduma hii wachezaji watapata mafao ya kipato pindi mchezaji atakapopata madhara ya kudumu au kupoteza maisha," alisema Sabi.

Alisema wakiwa kama mdhamini mkuu wa ligi hiyo, Benki ya NBC imejipanga kuhakikisha kwamba udhamini huo unagusa kila eneo linalohusu uboreshwaji wa mchezo huo ikiwamo kuzingatia suala zima la ustawi wa wachezaji ikiwa ni pamoja na suala la afya zao.

Hatua hiyo ya Benki ya NBC imeungwa mkono na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii chini ya Mwenyekiti, Stanslaus Nyongo ambapo kupitia hafla hiyo pamoja na kuwapongeza wadau alisema itasaidia kuboresha ubora wa ligi hiyo kwa kuwa wachezaji watacheza wakiwa huru na amani na hivyo kuonyesha viwango bora.

Kwa upande Rais wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), Wallace Karia, pamoja na kuipongeza benki hiyo na kampuni za Bima za Sanlam na Britam, alisema hatua hiyo ni ya kihistoria na kwamba inaunga mkono mkakati wa shirikisho hilo pamoja na serikali katika kukuza mchezo huo hapa nchini.

"Kwa hatua hii ya leo nadiliki kusema kwamba Benki ya NBC si tu ni mdhamini wa ligi kuu ya Tanzania Bara bali pia ni mshirika muhimu katika kukuza mchezo huu," alisema Karia.

Kwa upande wao Ofisa Mtendaji Mkuu wa Bima ya Sanlam, Hamis Suleiman pamoja na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Bima ya Britam, Ramond Komanga waliahidi kutoa huduma bora kwa walengwa hao ili waweze kutimiza wajibu wao vema pindi wanapokuwa uwanjani.




Katibu Mkuu Wizara ya Utamaduni Sanaa na Michezo, Dk. Hassan Abbasi, akizungumza wakati wa mafunzo ya hakimiliki kwa wahariri wa vyombo vya habari za michezo jijini Dar es Salaam jana, yalioandaliwa na Chama cha Hakimiliki Tanzania (COSOTA). **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Ruvu Shooting yaivutia kasi Polisi

**Na Shufaa Lyimo**

BENCHI la ufundi la Klabu ya Ruvu Shooting limesema linaendelea kujinoa kujiandaa kukutana na timu ya Polisi Tanzania, mchezo ambao utapigwa Aprili Mosi mwaka huu.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Kocha mkuu wa timu hiyo, Charles Boniface Mkwasa alisema anaupa umuhimu mkubwa mchezo huo.

"Timu ya Polisi ni miongoni mwa timu bora, kumbuka mchezo wake uliopita aliifunga timu ya Azam FC hivyo lazima tuingie kwa tahadhari," alisema Mkwasa.

Hata hivyo, alisema mchezo huo unatarajiwa kuwa mgumu na wenye ushindani na kudai anaendelea kuyafanyia kazi makosa ambayo ameyaona kwenye mchezo uliopita.

Alisema awali walipanga kucheza mchezo mmoja wa kirafiki lakini ilishindikana baada ya kukosa timu.

Alisema wachezaji wanaendelea vizuri na kudai hadi sasa ana majeruhi watatu ambao hali zao sio mbaya sana.

## Zimamoto kuiwashia moto Kisiwani

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

MAAFANDE wa Zimamoto watashuka dimbani leo katika mchezo wake wa 25 wa Ligi Kuu ya Zanzibar dhidi ya Kisiwani FC kutokea Pemba.

Mchezo huo utapigwa katika dimba la Amaan majira ya saa 10:00 jioni.

Zimamoto inaingia kwenye mchezo huo ikiwa nafasi ya sita katika msimu wa Ligi Kuu na alama zake 42, wakati wapinzani wao ni wakiwa tayari wameshashuka daraja huku wakiburuza mkia kwa alama zao tisa.

Akizungumza na gazeti hili Kocha wa Timu ya Zimamoto, Mohamed Hilali alisema licha ya kutoka katika mbio za ubingwa msimu huu, lakini matumaini yake makubwa yapo kumaliza ligi akiwa kwenye tatu bora.

Alisema msimu huu kwa timu yao haukuwa na mafanikio makubwa sana kama walivyotarajia na ili kutimiza robo ya mafanikio yao ni kumaliza ligi wakiwa katika nafasi tatu za juu.

Alisema kuelekea mchezo huo amejipanga kushinda na kupata alama tatu ili aweze kutimiza lengo lake.

Akiwazungumzia wapinzani wake, alisema licha ya kuwa tayari imeshashuka daraja haimaanishi kuwa haiwezi kupambana hivyo lazima wakacheza kwa tahadhari.

## Tanga City Marathon yatekeleza agizo

**Na Cheji Bakari, TANGA**

WAANDAAJI wa mashindano ya Tanga City Marathon wametekeleza agizo la Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Adam Malima la kuhakikisha wanawapatia medali washiriki 59 waliokosa medali hizo baada ya mashindano kumalizika Machi 27.

Malima alitoa siku saba kwa waandaaji hao kuhakikisha wanawapatia medali hizo washiriki wote waliokosa ambao walilalamika kufanyiwa utapeli wakati walitoa ada za usajili.

Mratibu wa mashindano hayo, Ali Mang'oro, alisema kuwa tayari ameshaandika barua kwa Ofisa Michezo wa Mkoa na nakala kuzipeleka kwa Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya ya Tanga, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tanga na Chama cha Riadha mkoa wa Tanga kueleza sababu ya changamoto na muda wa kuwakabidhi medali washiriki wote waliokosa.

"Tayari sisi kama waandaaji bali na kusikitishwa na tukio hilo, pia tumeshatekeleza agizo la Mkuu wa Mkoa la kuandika barua namna ya kuwakabidhi medali kwa washiriki wote waliokosa," alisema Mang'oro.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**BARCA KUMKOSA SALAH**
JARIBIO la Barcelona la kutaka kumsajili mshambuliaji wa Liverpool na Misri, Mohamed Salah mwenye umri wa miaka 29, linatarajiwa kugonga mwamba kwa sababu ya kubanwa na sheria za kifedha za LaLiga. ***(Mirror)***

**BELLINGHAM AGOMBEWA**
LIVERPOOL itakabiliwa na ushindani kutoka kwa Real Madrid katika mbio za kumsaka kiungo wa kati wa Borussia Dortmund, Jude Bellingham mwenye umri wa miaka 18. ***(Bild)***

**RAPHINHA APANGIWA BEI**
LEEDS United wamemuwekea dau la pauni milioni 67 winga wake wa Brazil, Raphinha mwenye umri wa miaka 25, huku Barcelona ikiwa tayari kulipa nusu ya kiwango hicho ***(Mirror)***

**LEED WABANA**
KLABU ya Leeds United imesisitiza kifungu pekee katika mkataba wa Raphinha kinachomruhusu kuondoka ni kile kinachosema aondoke kama watashushwa daraja kutoka Ligi Kuu ya England. ***(The Athletic)***

**OTAVIO AWANIWA**
MANCHESTER United, Liverpool na Newcastle zinataka kumsajili kiungo wa kati wa Ureno, Otavio mwenye umri wa miaka 27, kutoka Porto mwishoni mwa msimu. ***(A Bola)***

**MARTINEZ AWINDWA**
KLABU za Arsenal na Atletico Madrid zinaiwania saini ya mshambuliaji wa Argentina, Lautaro Martinez mwenye umri wa miaka 24, ambaye Inter Milan itamuuza iwapo itapata ofa ya pauni milioni 58 mwishoni mwa msimu. ***(Calciomercato)***

**CARVALHO ANUKIA LIVERPOOL**
LIVERPOOL imefikia makubaliano ya kumsajili mchezaji wa zamani wa timu ya taifa ya England chini ya miaka 18, Fabio Carvalho kutoka Fulham, baada ya kukaribia kabisa kumsajili kiungo huyo wa kati, mwenye miaka 19, wakati wa dirisha la uhamisho la mwezi Januari. ***(Football Insider)***

**SAKA KUONGEZEWA**
ARSENAL wanaandaa ofa ya kwanza ya kumuongeza mkataba winga wa England, Bukayo Saka mwenye umri wa miaka 20 mwisho wa msimu huu. ***(Fabrizio Romano)***

**DYBALA AITAKA ATLETICO**
MSHAMBULIAJI Paulo Dybala anataka kujiunga na Atletico Madrid mwishoni mwa msimu huu wakati mkataba wake na Juventus utakapomalizika - na ingawa Inter Milan pia wanataka kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, wanaweza kufanya hivyo iwapo watamuuza raia mwenzake wa Argentina, Lautaro Martinez. ***(Mundo Deportivo)***

**PEPE KUONDOKA**
WINGA wa Ivory Coast, Nicolas Pepe, mwenye umri wa miaka 26, amedokeza kuhusu uwezekano wa kuondoka Arsenal mwishoni mwa msimu, miaka mitatu baada ya kutua kwa uhamisho wake ulioweka rekodi ya klabu wa pauni milioni 72. (Sun)

**KETELAERE ATAKIWA**
KLABU ya Leicester City imekuwa ikihusishwa na mshambuliaji wa Club Bruges, Charles de Ketelaere. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21 amepachika mabao 17 katika mechi 41 msimu huu na kucheza mechi yake ya tano na timu ya taifa ya Ubelgiji katika mchezo wa kirafiki mwishoni mwa wiki iliyopita dhidi ya Jamhuri ya Ireland. ***(Leicester Mercury)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# LAPORTA: HATUWAWEZI HAALAND NA MBAPPE

Asema kama wao wenyewe wakitaka kuichezea Barcelona sawa, lakini mishahara itakuwa ngumu kwao...

**BARCELONA, Hispania**

JOAN Laporta angetamani kumsajili ama Erling Haaland au Kylian Mbappe - lakini ikiwa tu wangetaka kujiunga na Barcelona na kuwasilisha mahitaji ya busara zaidi ya kifedha.

Haaland na Mbappe wanaweza kuhama mwishoni mwa msimu huu, huku klabu kubwa zaidi za Ulaya zikijiweka katika nafasi nzuri ya kuwasajili washambuliaji hao bora wa kizazi chao.

Haaland ana kipengele cha kutolewa kwa euro milioni 75 huko Borussia Dortmund, wakati mkataba wa Mbappe wa Paris Saint-Germain utamalizika mwishoni mwa msimu huu.

Lakini kuwasajili wachezaji hao kutahitajika gharama kubwa katika suala la mishahara na ada za mawakala.

Kwa sababu hiyo, rais wa Barca, Laporta anatatizika kuona ni jinsi gani anaweza kuwasajili nyota hao kutua Camp Nou.

"Haaland au Mbappe? Ikibidi nichague, ningeshikilia kile ambacho nimesema wazi," Laporta aliiambia RACI.

"Yule anayeweka wazi kuwa anataka kuichezea Barca, ndiye anayetakiwa kuja hapa.

"Kwa muda huu hakuna hata mmoja kati ya hao wawili aliyenieleza hivyo, wasipojisikia itakuwa ngumu.

"Kilichoelezwa kwangu ni masharti kuhusu mikataba hii miwili. Hatutakubali kamwe kutumia takwimu hizo, la hasha."

Vizuizi vya kifedha vya Barcelona vilisababisha kuachiliwa kwa Lionel Messi kwenda PSG mwaka jana, na wazo la kumrudisha mshindi huyo mara saba wa Ballon d'Or pia lilikataliwa na Laporta.

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 1,089

MECHI KALI
TIVERTON TOWN
VERSUS
WESTON SUPER MARE
1 | 2.39
X | 3.55
2 | 2.70

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# VAN GAAL AMUONYA TEN HAG KWENDA MAN UTD



**AMSTERDAM, Uholanzi**

KOCHA wa zamani wa Manchester United, Louis van Gaal amemuonya Erikten Hag dhidi ya kuchukua mikoba ya ukocha pale Old Trafford msimu huu wa joto.

Akizungumza katika mkutano wa wanahabari kabla ya mechi ya kirafiki ya Uholanzi dhidi ya Ujerumani, Van Gaal alisema kocha anayehitajika wa Ajax "anapaswa kuchagua klabu ya soka, si klabu ya kibiashara."

Van Gaal alitumia miaka miwili kwenye dimba la Old Trafford kati ya 2014 na 2016, na kuiletea klabu hiyo taji lao la kwanza kuu tangu kustaafu kwa Alex Ferguson alipoiongoza kutwaa Kombe la FA mwaka 2016.

Huku kocha wa muda wa Mashetani Wekundu hao, Ralf Rangnick akitarajiwa kuachia wadhifa huo ili kuangazia kazi ya ushauri na klabu baada ya msimu ambao haukuwa na matokeo mazuri, Van Gaal amemuonya Ten Hag, ambaye anachukuliwa kuwa mmoja wa walio mstari wa mbele katika nafasi hiyo, dhidi ya kuhamia klabu hiyo. Manchester.

United wameripotiwa kuwa tayari wameshafanya mawasiliano na kocha huyo wa Ajax, ambaye Van Gaal alimtaja kama "kocha mkuu".

Hata hivyo, Van Gaal haamini kwamba uhamisho huo utakuwa bora zaidi kwa Ten Hag katika maisha yake ya soka.

"Nadhani Ten Hag ni kocha mzuri; nilisema hivyo mara nyingi," Van Gaal alisema.

"Kocha mkubwa ni mzuri kwa Man United. Lakini Man United ni klabu ya kibiashara.

"Hayo ni maamuzi magumu kwa kocha. Kama kocha, unapaswa kupendelea klabu ya soka.

"Sitaandamana na kazi yake. Akitaka hivyo atanipigia simu, tunazungumza sisi kwa sisi.

"Anapaswa kuchagua klabu ya soka, si klabu ya kibiashara."

Van Gaal alikuwa mkosoaji mkubwa wa shughuli za kibiashara za United wakati alipokuwa na klabu hiyo, akisikitikia madhara ya kimwili ya ziara ya kujiandaa na msimu mpya katika msimu wake wa kwanza wa majira ya joto mwaka 2014.

Ten Hag ameshinda mechi 153 kati ya 207 akiinoa Ajax katika mashindano yote, lakini mwezi uliopita alitolewa kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya na Benfica.

# Silva: Kumpoteza Azpilicueta ni pigo

**LONDON, England**

THIAGO Silva amekiri kuwa itakuwa pigo kubwa ikiwa Chelsea itapoteza ujuzi wa uongozi wa Cesar Azpilicueta mwishoni mwa msimu huu.

Blues hao wakiwa katika hali ya sintofahamu huku wamiliki watarajiwa wakiomba kuinunua klabu, mikataba mipya kwa wachezaji inaonekana kuwa tatizo.

Hilo linaweka uwezekano mkubwa kwamba nahodha Azpilicueta, pamoja na walinzi wenzake Andreas Christensen na Antonio Rudiger, watondoka hapo Stamford Bridge kama wachezaji huru mikataba yao itakapokamilika mwishoni mwa msimu huu. Naye Silva mwenye umri wa miaka 37, amesisitiza kuondoka kwa Mhispania huyo kutaacha pengo kubwa katika kikosi cha kocha Thomas Tuchel.

Mbrazil huyo alisema: "Yeye ni kijana wa kuvutia, mtaalamu wa hali ya juu ambaye bila shaka anastahili kuwa hapo alipo na kuvaa kitambaa, ambacho kina maana kubwa kwake.

"Kuna manahodha wa aina tofauti, wapo wanaozungumza zaidi na wengine kimya lakini wana maana kubwa kwa timu. "Azpilicueta ana vipengele vyote viwili. Ni muhimu sana uwanjani na nje anaikutanisha timu inapobidi kuzungumza na kuweka mambo wazi ili yasiharibike."

Silva alisaini nyongeza ya mwaka mmoja Januari ili kumfunga hapo Blues hadi mwisho wa msimu ujao.

Beki huyo mkongwe ameonekana kuwa na mafanikio makubwa tangu alipojiunga kwa uhamisho wa bila malipo Agosti 2020 baada ya mkataba wake na Paris Saint-Germain kumalizika.

9,062,840

# IDD ASHINDA SH. MILIONI 19 JACKPOT BONUS SPORTPESA

**NA Mwandishi Wetu**

MKAZI wa Kunduchi Wilaya ya Kinondoni eneo la Mtongani, Idd Juma Hamisi, ameshinda shilingi 19,493,189 katika Jackpot Bonus ya Sportpesa iliyochezwa mwishoni mwa wiki, baada ya kupatia kwa usahihi mechi 12 kati ya mechi 13.

Akizungumza baada ya makabidhiano ya mfano wa hundi katika ofisi za Sportpesa jijini Dar Es Salaam, Idd amesema alianza kucheza na Sportpesa miaka kadhaa iliyopita, baada ya kuona marafiki zake wanashinda.

"Nakumbuka nilianza kucheza Sportpesa baada ya kwenda Nachingwea kikazi na siku niliyofika katika eneo nililofikia pale sikuwakuta wenyeji wangu. Baada ya kuulizia niliambia wameenda kutoa hela zao walizoshinda mikeka."

"Baada ya hapo mmoja kati ya hao jamaa zangu alinipakulia app ya Sportpesa na kuiweka kwenye simu yangu na kisha kunifundisha namna ya kucheza. Kuanzia hapo mpaka leo naweza kusema mimi ni mmoja wa wachezaji watiifu kabisa wa Sportpesa," alisema Idd.




Akielezea namna alivyopata ushindi huo wa Jackpot bonus, alisema aliweka mkeka wake siku ya Jumamosi baada ya kuuchambua kwa siku tano mfululizo.

"Jackpot hii niliyoshinda niliweka zaidi ya mikeka 10 hivi. Mimi kwa kawaida Jackpot moja ikiisha huwa naanza kufuatilia Jackpot inayofuatia. Baada ya kuona mechi za Jackpoti hii niliyoshinda, nilijaribu kwanza siku ya Jumatatu na kuweka mkeka wa kwanza.

Anaendelea kueleza kuwa ilipofika Jumamosi asubuhi aliweka mikeka yake yote iliyobakia na kuamua kusubiria hatima kwa kuangalia kwenye luninga.

"Unajua siku ya Jumamosi kwanza katika mechi kumi nilipata mechi 9 na kukosa moja. Kitendo hicho kilinipa hamasa ya kufuatilia matokeo ya timu zilizobaki. Siku ya Jumapili nilitenga laki 6 ili nilinde mtaji wangu niliotumia."

Akizungumzia ushindi huo Meneja Uhusiano wa Sportpesa, Sabrina Msuya, alimpongeza Idd kwa ushindi wa Jackpot Bonus na pia aliwataka Watanzania waendelee kuipambania Jackpoti. Kwa wiki hii Jackpot imesimamia Sh. 1,089,062,840

Sambamba na hilo aliwaomba Watanzania kuendelea kucheza kila siku ili waingie kwenye droo ya Bet Bonanza ambapo leo ni wiki ya tatu na washindi wa milioni moja moja wanapatikana.

# Namungo yarejea nchini kuiwinda KMC

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya Namungo ambayo ilikuwa nchini Zambia kwa ajili ya ziara fupi na mechi kadhaa za kirafiki imerejea nchini na tayari imeanza mazoezi kwa ajili ya mechi yake ya Ligi Kuu dhidi ya KMC.

Kocha Msaidizi wa klabu hiyo, Jamhuri Kihwelo 'Julio', amesema kuwa ziara ya nchini Zambia ilikuwa kwanza kuwapumzisha wachezaji wao ili kubadilisha mazingira kutoka sehemu moja kwenda nyingine, lakini kujisikia kuwa ni watu wanaothaminiwa na klabu yao.

"Lengo ilikuwa ni kuwapumzisha vijana na kuwafanya waone wanathaminiwa, pia kutoka sehemu moja kwenda nyingine akili inapumzika. Tumecheza mechi tatu za kirafiki na tumerejea nchini, tumeshaanza mazoezi ya kujiandaa na mechi yetu dhidi ya KMC. Najua itakuwa mechi ngumu sana kwa sababu wamepoteza mechi kama tatu hivi, kwa hiyo hawatokubali kupoteza tena kirahisi, na sisi tunataka tushinde ili kujiweka kwenye mazingira mazuri kwenye timu nne za juu," alisema Julio.

Namungo itakuwa jijini Dare es Salaam ama Uwanja wa Uhuru, au Azam Complex, ikiwa mgeni wa KMC kwenye raundi ya 19 ya mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara.

Namungo inakamata nafasi ya nne kwenye Ligi Kuu, ikiwa na pointi 25 kwenye mechi 18 ilizocheza, huku wenyeji wao wakiwa kwenye nafasi ya saba ikiwa na pointi 22.

Ikiwa nchini Zambia, Namungo ilicheza mechi mbili za kirafiki za kimataifa, ikichapwa mabao 3-2 dhidi ya Lusaka Dynamos, ikatoka sare ya mabao 2-2 dhidi ya Green Buffaloes.

# JACKPOT MECHI WIKI HII

**BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13**

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 02/04/22 | 17:00 | Leeds vs Southampton | 2.36 | 3.53 | 2.83 |
| 02. 02/04/22 | 17:00 | Wolverhampton vs Aston Villa | 2.84 | 3.09 | 2.54 |
| 03. 02/04/22 | 19:30 | Borussia Dortmund vs RB Leipzig | 2.38 | 3.59 | 2.69 |
| 04. 03/04/22 | 14:00 | Rangers vs Celtic | 2.36 | 3.28 | 2.88 |
| 05. 03/04/22 | 15:30 | Fortuna Sittard vs Heracles Almelo | 2.58 | 3.28 | 2.58 |
| 06. 03/04/22 | 16:00 | Troyes vs Reims | 2.56 | 2.96 | 2.96 |
| 07. 03/04/22 | 16:00 | Clermont Foot vs Nantes | 2.55 | 3.05 | 2.90 |
| 08. 03/04/22 | 16:00 | Atalanta vs Napoli | 2.42 | 3.20 | 2.90 |
| 09. 03/04/22 | 16:30 | Augsburg vs VfL Wolfsburg | 2.86 | 3.26 | 2.45 |
| 10. 03/04/22 | 19:00 | Panathinaikos vs PAOK | 2.59 | 3.03 | 2.79 |
| 11. 03/04/22 | 19:30 | Granada vs Rayo Vallecano | 2.68 | 3.13 | 2.73 |
| 12. 03/04/22 | 20:00 | Moreirense vs Vitoria Guimaraes | 2.80 | 3.20 | 2.47 |
| 13. 03/04/22 | 21:45 | Juventus vs Inter | 2.70 | 3.25 | 2.55 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## JUMATANO - 30/03/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 1186 | Uganda Revenue Authority FC vs Dove All Stars | 1.70 | 3.45 | 4.48 |
| 14:00 | 3494 | Sariyer vs Osmanlispor | 2.28 | 3.32 | 2.78 |
| 14:00 | 4376 | Sanliurfaspor vs Tarsus | 2.92 | 3.01 | 2.35 |
| 14:00 | 4560 | Eskisehirspor vs Akhisar Bld | 3.60 | 3.25 | 1.94 |
| 14:15 | 2412 | Arema vs PSM Makassar | 1.73 | 3.41 | 4.39 |
| 14:45 | 1323 | Saipa Karadj vs Mes Shahr-e Babak | 2.01 | 2.95 | 4.20 |
| 14:45 | 2207 | Machine Sazi Tabriz vs Vista Turbine | 5.05 | 2.92 | 1.79 |
| 14:45 | 3369 | Arman Gohar Sirjan vs Rayka Babol | 1.83 | 3.20 | 4.80 |
| 14:45 | 3942 | Shahrdari Hamedan vs Ghasghaei Shiraz | 2.32 | 2.70 | 3.75 |
| 14:45 | 4514 | Shams Azar Qazvin vs Pars Jonoubi Jam | 3.20 | 2.60 | 2.65 |
| 14:45 | 5009 | Khosheh Talaei vs Kheybar Khorramabad FC | 3.12 | 2.73 | 2.42 |
| 14:45 | 5180 | Malavan Bandar Anzali vs Shahrdari Astara | 1.46 | 3.59 | 7.38 |
| 15:00 | 2368 | Saint George FC vs Sebeta City FC | 1.65 | 3.50 | 4.77 |
| 15:00 | 3458 | Rhodos FC vs Levadiakos | 8.76 | 3.75 | 1.39 |
| 15:00 | 3543 | FC Veria vs PO Triglias | 1.43 | 3.95 | 8.40 |
| 15:00 | 5411 | Thesprotos vs AO Trikala | 1.31 | 4.28 | 9.53 |
| 15:15 | 2255 | Shahin Bushehr vs Esteghlal Khuzestan | 6.60 | 3.05 | 1.69 |
| 15:15 | 3987 | Esteghlal Mollasani vs Sanat Mes Kerman FC | 3.95 | 2.70 | 2.24 |
| 15:30 | 2309 | Palermo vs Taranto Sport | 1.61 | 3.70 | 5.60 |
| 15:30 | 2838 | SKODA Xanthi vs AE Larissa | 2.73 | 2.63 | 2.83 |
| 16:00 | 1385 | Wakiso Giants FC vs SC Villa | 2.18 | 3.10 | 3.45 |
| 16:00 | 1453 | Jedinstvo BP vs Bokelj | 1.55 | 3.54 | 5.81 |
| 16:00 | 1724 | FK Sloboda Novi Grad vs FK Buducnost Pilica | 1.11 | 7.40 | 15.58 |
| 16:00 | 3347 | FK Cetinje vs OFK Titograd | 2.62 | 2.86 | 2.71 |
| 16:00 | 3720 | FK Sutjeska Foca vs FK Podrinje | 1.16 | 5.86 | 14.64 |
| 16:00 | 3857 | Grbalj vs OFK Igalo 1929 | 3.88 | 3.16 | 1.90 |
| 16:00 | 4830 | Busoga United vs Tooro United | 1.69 | 3.50 | 4.47 |
| 16:00 | 5253 | Zesco United vs Prison Leopards | 1.73 | 3.21 | 4.76 |
| 16:00 | 5527 | Berane vs FK Arsenal Tivat | 3.64 | 2.91 | 2.08 |
| 16:00 | 5712 | Kom vs Mladost DG | 2.08 | 3.07 | 3.41 |
| 16:00 | 5863 | Konkola Blades vs Kansanshi Dynamos | 2.81 | 2.57 | 2.81 |
| 16:30 | 5348 | FK Sloga Doboj vs FK Zeljeznicar Banjaluka | 1.40 | 3.99 | 7.39 |
| 16:45 | 4721 | Persebaya Surabaya vs Pusamania Borneo | 2.18 | 2.91 | 3.35 |
| 17:00 | 5623 | FK Loznica vs FK Imt Novi Beograd | 2.65 | 3.05 | 2.70 |
| 17:30 | 3147 | FK Zbuzany vs Zivanice | 2.30 | 3.60 | 2.58 |
| 18:00 | 3204 | Hadiya Hosahina FC vs Fasil Kenema | 4.66 | 2.96 | 1.83 |
| 18:35 | 2957 | Hajer Club vs Al Orubah | 2.18 | 2.92 | 3.35 |
| 18:45 | 4132 | AL Kawkab vs Al Qadisiyah | 3.20 | 2.91 | 2.25 |
| 19:00 | 2047 | FK Atmosphere vs Riteriai B | 3.02 | 3.65 | 2.02 |
| 19:00 | 3356 | AZ Picerno vs Campobasso Calcio | 2.26 | 3.00 | 3.40 |
| 19:15 | 4667 | Al Wehda vs Bisha FC | 1.45 | 3.83 | 6.60 |
| 19:15 | 5777 | Jeddah Club vs Alshoulla | 2.78 | 2.78 | 2.63 |
| 20:30 | 2453 | RW Oberhausen vs Sportfreunde Lotte | 1.44 | 4.28 | 5.83 |
| 21:00 | 4489 | Felanitx vs CD Manacor | 6.22 | 3.89 | 1.47 |
| 21:45 | 1436 | Tiverton Town vs Weston Super Mare | 2.39 | 3.55 | 2.70 |
| 21:45 | 2644 | Truro City vs Merthyr Town | 1.42 | 4.18 | 6.41 |
| 22:00 | 2612 | Mallorca B vs CF Soller | 1.25 | 5.40 | 11.00 |
| 22:00 | 3930 | Envigado FC vs Atletico Bucaramanga | 2.11 | 2.97 | 3.45 |
| 23:00 | 3877 | Union Magdalena SM vs Real Santander | 1.40 | 3.98 | 7.56 |
| 23:30 | 5066 | Club Cortulua vs Fortaleza (COL) | 1.66 | 3.26 | 5.26 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo


Jumatano Machi 30, 2022

Nipashe






## Laporta: Hatuwawezi Haaland na Mbappe




Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NBC, Theobald Sabi na Rais wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), Wallace Karia (katikati), wakiwa pamoja baada ya kusaini mikataba ya makubaliano ya kiutendaji kuhusu huduma mpya ya Bima kwa wanamichezo. **PICHA: TFF**

# PABLO BADO YUPO SANA SIMBA SC

●●●Yasema taarifa ya kwamba wanataka kumfukuza ni uzushi na zimeanzishwa kwa lengo la kupoteza utulivu...

**Na Adam Fungamwango**

HUKU ikiwa kwenye maandalizi makali kujiandaa mechi ya mwisho ya Kundi D, Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya US Gendamarie ya Niger Jumapili kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, klabu ya Simba imewataka wanachama na mashabiki wake, kupuuza taarifa kuwa wapo mbioni kumfukuza Kocha Mkuu Pablo Franco.

Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally amesema kuwa taarifa hizo ni za kutungwa na zimeanzishwa makusudi na baadhi ya watu wasioitakia mema klabu hiyo, zikiwa na lengo la kupoteza utulivu.

Akizungumza jijini Dar es Salaam, Ahmed alisema kuwa ni kweli walimpa kocha huyo raia wa Hispania malengo ya kuifikisha nusu fainali, lakini hakuna sehemu yoyote waliyowahi kumwambia kuwa asipowafikisha watamtimua.

"Lengo la taarifa hizo za kutungwa ni kwa ajili ya kupoteza utulivu ndani ya klabu, hasa kuelekea kwenye pambano hilo muhimu. Ni kweli kocha tulimpa malengo ya kuifikisha timu nusu fainali, lakini hatukumwambia tusipofika tutamfukuza," alisema.

"Ikitokea tukifika tutafurahi kwa sababu tumeweza kufikia malengo, lakini ikitokea tumekwama tutakaa chini na mwalimu tutamuuliza amekwama wapi atatuambia au atatupa sababu zake, na uongozi utakaa na kuzifanyia kazi, baada ya hapo maamuzi ya kimaslahi ya pande mbili yataamualiwa, lakini kwa sasa bado ni kocha wetu, hana wasiwasi na tunamuamini, ameleta mafanikio makubwa sana kwenye kikosi cha Simba kwa timu nzima na mchezaji mmoja mmoja, kuna sababu gani ya kumuwekea presha?" Alihoji Meneja huyo.

Alisema siku zote kwenye soka kocha anaweza asitimize malengo aliyowekewa, lakini viongozi wakawa na imani naye kwa sababu ya kuitengeneza timu imara, akaendelea kuwepo, lakini unaweza ukawa na kocha aliyetimiza malengo, lakini akafukuzwa kwa sababu kila mkiangalia viongozi mnaona hakuna muendelezo kwenye kikosi na hakuchezi vema." Alisema.

Simba inakwenda kucheza dhidi ya US Gendamarie kwenye mechi ambayo iwapo itashinda itakwenda moja kwa moja kwenye hatua ya robo fainali, huku kukiwa pia na tetesi zikizuka kuwa iwapo ikishindwa kufuza basi, ataonyeshwa mlango wa kutokea.

# Yanga na Mafunzo kufunzana Chamazi leo

**Na Adam Fungamwango**

VINARA wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga leo saa moja usiku itakuwa kwenye Uwanja wa Azam Complex kucheza mechi ya kirafiki dhidi ya Mafunzo ya Zanzibar.

Ofisa Habari wa klabu hiyo, Hassan Bumbuli amesema kuwa ni mechi ambayo iliombwa na Kocha Mkuu Nasreddine Nabi kwa ajili ya kuendelea kuwaweka fiti wachezaji wake, hasa baada ya mapumziko kupisha kalenda ya Shirikisho la Soka Duniani (FIFA).

Ni mechi ambayo pia huenda mashabiki wakashuhudia urejeo wa winga Jesus Moloko aliyekuwa majeruhi, lakini kwa sasa amepima kabisa na kurejea uwanjani.

"Kocha wetu ametaka mechi hii kwa ajili ya kuendelea kuwapa wachezaji utimamu wa mwili, lakini pia tumesikia kilio cha wanachama na mashabiki wa Yanga ambao wanasema hawataki kukaa muda mrefu bila kuiona timu yao ikicheza, kwa hiyo leo saa moja usiku tuko Chamazi, tukajumuike kule, tujazane ili tujue tarehe sita tukicheza na Azam Aprili 6 tujue tutakaaje," alisema Bumbuli.

Kuhusu mechi ya kirafiki Bumbuli alisema kuwa wameamua kucheza na Mafunzo kwa sababu hawajawahi kucheza nayo, hivyo watapata kitu kipya, tofauti na timu zingine za Bara na Visiwani ambazo nyingi tayari wameshakutana nazo.

"Tumecheza na timu nyingi za Zanzibar, lakini hatujawahi kucheza na Mafunzo kwa muda mrefu, tumeona tucheze nayo kwa sababu huenda inaweza kutupa kitu kipya ambacho hatujawahi kukutana nacho na tukajifunza, na hizi za Tanzania Bara, karibuni zote tumecheza nazo kwenye mzunguko wa kwanza, kwa hiyo hatukuona kipya tutakachokwenda kujifunza kutoka kwao," alisema.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >